**EWURA** yafungia vituo tuhuma za kuficha mafuta



UKURASA 3

**Ajali** ya treni na gari la magereza yaua na kujeruhi

UKURASA 3



**CHADEMA** yaibua hoja uboreshaji daftari la wapigakura

UKURASA 4


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 1, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581450

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



tigo pesa
SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#


# Samia ataka viongozi kuiga mfano wa Dk. Salim

• **Warioba** afichua alivyobezwa baada Nyerere kumteua lakini...

*Endelea Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimjulia hali Waziri Mkuu mstaafu, Dk. Salim Ahmed Salim, nyumbani kwake, Oysterbay Dar es Salaam jana, baada ya uzinduzi wa Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka za Kumbukumbu za Kidijitali za kiongozi huyo, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC). **PICHA: IKULU**



Papa Francis akimsimika Askofu Mkuu Mwandamizi wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Tabora, Protase Rugambwa kuwa Kardinali katika kanisa la Mt. Peter Basilica mjini Vatcan, jana. **PICHA: REUTERS**

## Papa Francis amsimika rasmi Rugambwa kuwa Kardinali


UK. 17

## Madereva wa bodaboda wagoma kumzika mwenzao kisa rambirambi

UKURASA 3



MICHEZO NI ZAMU YA SIMBA, SINGIDA FG CAF UK.24 MAONI, KATUNI UK.6




Mohamedi Saidi (81) mkazi wa Buguruni, jijini Dar es Salaam, akitoa maelezo kwa Dk. Sigfrid Shayo (kulia) wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), baada ya kufika katika hospitali ya Dar Group-JKCI jana, kwa ajili ya kupatiwa huduma ya vipimo na matibabu bure, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Samia ataka viongozi kuiga mfano wa Dk. Salim

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemmwagia sifa kemkem Waziri Mkuu mstaafu, Balozi Dk. Salim Ahmed Salim, huku akitaka viongozi kuiga mfano wake katika uongozi ikiwa ni hatua ya kumuenzi mwanadiplomasia huyo mkongwe.

Pamoja na kummwagia sifa hizo, Rais Samia amekibadilisha jina Chuo cha Diplomasia kuwa na jina la Dk. Salim ikiwa ni hatua ya kumuenzi kutokana na utumishi wake ndani na nje ya nchi.

Hatua ya kubadili jina la chuo hicho, aliitangaza jana katika hafla ya uzinduzi wa tovuti ya nyaraka za Dk. Salim iliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Dk. Salim ni mwanadiplomasia mashuhuri aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tano na Katibu Mkuu wa Nane wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) kuanzia mwaka 1989 - 2001 (sasa Umoja wa Afrika).

Uzinduzi huo ulihudhuriwa pia na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Naibu Spika, Mussa Zungu, mawaziri na naibu mawaziri na viongozi wengine wastaafu akiwamo Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete.

Katika uzinduzi huo, Dk. Salim hakuhudhuria kutokana na matatizo ya kiafya na kuwakilishwa na wanafamilia wakiongozwa na mtoto wake, Ahmed Salim.

"Kwa sababu mcheza kwao hutunzwa, na tumesema alikuwa mwanadiplomasia mahiri, tumekubaliana kukipa Chuo kile cha Diplomasia jina. Na sasa rasmi kitakuwa kinaitwa Dk. Salim Ahmed Salim Centre for Foreign Relations," alisema.

Lengo la kukipa jina hilo, alisema ni kuonyesha mchango uliotolewa na mwanadiplomasia huyo mahiri ambaye alifanya kazi kwa muda mrefu katika nyanja ya kidiplomasia ya kimataifa na kwa nidhamu bila kukata tamaa.

Alisema Dk. Salim alithamini elimu katika jamii na amesaidia wengi kufikia maendeleo na ndoto zao kwa kutoa ushauri na mafundisho mbalimbali.

Alisema katika uongozi wake, Dk. Salim alitoa mchango mkubwa katika uhamasishaji wa masuala ya uzalendo, muungano na umoja ambayo yalichangia katika kudumisha amani na umoja wa taifa.

Kutokana na mchango mkubwa alioutoa kwa taifa na kimataifa, Rais Samia alitoa wito kwa viongozi wa umma kuiga mfano wake kwa kutunza kumbukumbu za maisha yao, badala ya kuzichoma moto.

Alisema wazitunze kwa manufaa ya vizazi vya sasa na baadaye ili zisaidie kukuza na kuimarisha uelewa wa juhudi za kila kiongozi, historia ya nchi na bara la Afrika.

"Shughuli hii imetufumbua macho ya kuweka kumbukumbu muhimu, ndiyo maana mmemsikia Waziri (George) Simbawawene (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) hapa anasema 'tuna maktaba tutaiongezea fedha kufanya shughuli hii' nami nitie baraka kwenye hilo na niseme mwendelee kufanya hivyo," alisema.

Rais Samia alisema anafahamu Taasisi ya Uongozi ina mradi wa tawasifu wa viongozi wakuu wa nchi na barani Afrika, ambapo hadi sasa wameshatoa vitabu viwili vya viongozi wakuu wa serikali, Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi na Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

Alisema anaelewa kwamba Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, yuko kwenye jitihada kubwa ya kuandika kitabu chake kwa nguvu zake na kuwataka waanzie hapo, yale yanayowezekana kuwekwa kwenye dijitali yakae huko.

"Lakini mumsaidie amalize kitabu chake na yeye aingie kwenye hiyo tovuti. Nimefahamishwa nyingine mbili ambazo mnazitayarisha ni za viongozi mawaziri wakuu wastaafu, kaka yetu marehemu Edward Moringe Sokoine na baba yetu, Rashid Kawawa. Hizi ni jitihada nzuri za kuhifadhi kumbukumbu za viongozi wetu lakini twende kwenye mwelekeo huu ambao familia ya Dk. Salim wametuonyesha," alisema.

Rais pia aliagiza waende kutengeneza tovuti ya serikali ya kuweka kumbukumbu ya viongozi kama walivyoonyeshwa na Dk. Salim.

Mtoto wa Dk. Salim, Ahmed, kwa niaba ya familia, alimshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa ambayo imefanyika hadi kufanikisha uzinduzi wa tovuti hiyo.

Alibainisha kwamba mradi huo waliuanza tangu mwezi Oktoba mwaka 2021 kwa kupitia nyaraka nyingi muhimu ambazo zimeingia ndani ya tovuti hiyo.

Waziri Simbachawene alisema Taasisi ya Uongozi ambayo moja ya eneo ni kufanya utafiti mbalimbali na ndiyo iliyosimamia utungwaji wa vitabu vinavyohusu viongozi na ndiyo imesimamia eneo la ufundi lauhifadhi wa kumbukumbu kidijitali.

"Mwelekeo wetu ni nini? Tumejifunza kumbe jambo hili linaweza kufanyika kwa viongozi wengine kwa hivyo, uwezo wa serikali upo vizuri katika utunzaji wa kumbukumbu, tunayo idara ambayo inatunza kumbukumbu na nyaraka, tumejenga ofisi nzuri kule Dodoma na tunatunza makavazi mbalimbali," alisema.

Simbachawene alisema bajeti ya mwaka huu wataongeza uwezo wa kidijitali katika kuhifadhi nyaraka na yeyote atakayehitaji kuhifadhiwa ataweza kufanya hivyo.

"Mheshimiwa Rais kama ikikupendeza tuanze na viongozi hawa wakuu kama tunavyolifanya hili basi tufanye kwa viongozi wote wakiwa hai waweze kushiriki katika matukio kama haya yanayotambua mchango wao," alisema.

# ... Warioba afunguka alipoteuliwa Waziri Mkuu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amesema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alipomteua Dk. Salim Ahmed Salim kuwa Waziri Mkuu, viongozi wengi hasa wa Tanzania Bara, walisema ameboronga hawezi kumteua mswahili wa mjini.

Jaji Warioba aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka ya Dk. Salim, iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi wa serikali na wastaafu.

Katika mjadala uliooendeshwa na mwezeshaji Prof. Saida Yahya-Othman, ambao Jaji Warioba alikuwa miongoni, alipotakiwa amzungumzie Dk. Salim alikuwaje kama Waziri Mkuu, ndipo alipofunguka hayo.

Jaji Warioba alianza kwa kusema kuwa, Dk. Salim ni mtu mwenye uwezo, makini, mwenye upeo mpana na maisha yake yote ameyatumia kujifunza na kusoma vitabu na magazeti.

"Waliopata bahati kufika ofisini kwake (enzi hizo) utakuta ana rundo la magazeti ya ndani na ya nje, anasikiliza taarifa, ukifika wakati wa habari anaangalia habari. Kama anatoa hoja, kwa kitu amejifunza akisema kitu, atasema kwa ufasaha bila kumtazama mtu. Alisema Dk. Salim akiwa na hoja yake, alikuwa haogopi na alikuwa hamtazami huyu ni mtu wa namna gani.

"Nimeombwa nizungumze Salim alikuaje kama Waziri Mkuu. Mwaka 1984 Mwalimu Nyerere alivyomteua kuwa Waziri Mkuu, kulikuwa na viongozi wengi tu hasa wa Bara, walisema hapa Mwalimu ameboronga, hawezi kumteua mswahili wa mjini ambaye amekaa nje muda mrefu hajui matatizo ya nchi hii akawa Waziri Mkuu, hataweza kusukuma maendeleo," alisimulia Jaji Warioba.

Alisema Mwalimu alikuwa anajua uwezo wa Dk. Salim ndiyo maana alimteua na alipokuwa Waziri Mkuu alishangaza wengi kwa kuwa alikuwa mtu wa kujifunza na ndani ya muda mfupi alijifunza mengi.

Alisema ndani ya muda mfupi alizunguka nchini akaelewa matatizo na alikuwa akienda mahali popote na kukuta kuna tatizo ambalo ni la utendaji alihitaji sera, akitoka huko alikuwa anatoa maelekezo ya nini kifanywe.

"Niwape mfano, alifanya ziara Lindi na Mtwara alipofika kule alikuta hali ni mbaya sana, moja wapo ilikuwa ni mavazi, watu hawana mavazi wengine wanavaa kama magunia hivi.

"Alipotoka huko hata hakungojea kuripoti kwa Mwalimu alitoa maelekezo kwamba, hili suala ni la utendaji nguo zitafutwe zipelekwe mara moja Kusini na ilifanyika hivyo, alikuwa si mtu wa maneno, bali na vitendo pia,"alisema Jaji Warioba.

Alisema miezi 19 ambayo alikuwa Waziri Mkuu kulikuwa na matokeo chanya kwa kuwa alikuwa ni mtu mwenye kuweka kumbukumbu.

"Kama mnavyosema, kwenye tovuti mtaona zipo kumbukumbu za aina nyingi pamoja na maandishi yake, pahali popote kama palikuwa na mazungumzo kwenye vikao, (Dk) Salim alikuwa anaandika, mwaka 1976 Mwalimu alitutuma Geneva mimi na Salim, tulikaa wiki sita katika mazungumzo yale wakati mwingine inafika Mwenyekiti anabadili gia yake angani.

Anasimulia kuwa siku moja mwenyekiti ambaye alikuwa ni Muingereza alikwenda na msimamo wake lakini Dk. Salim kutokana na kuandika alimwambia, "Mwenyekiti si tulikubaliana hivi".

Jaji Warioba alisema Dk. Salim alipokuwa Waziri Mkuu aliratibu ofisi ile kuwa na uongozi jumuishi wa kimatendo alikuwa na maofisa kama saba kila mmoja akiwa na kitengo akifuatilia na kumpa mrejesho wa utendaji wa kila wizara.

"Wale waliosema Mwalimu ameboronga wakaanza kupata joto kwa kuwa kila wakati alikuwa anamfuta mtu "Hii unatekelezaje" huu utaratibu ndiyo niliukuta nikauimarisha ulisaidia sana.

"Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa ni waratibu wa shughuli za serikali, aliweka utaratibu ambao unaratibu shughuli za serikali kwa ujumla ndipo walipojua uwezo wa (Dk.) Salim," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Madereva bodaboda wagoma kumzika mwenzao kisa michango ya rambirambi

**Na Said Sindo,** GEITA

WAENDESHA bodaboda mjini hapa wamegoma kufanya maziko ya mwili wa mwenzao, Doto Abel, mkazi wa Nyantorotoro kwa madai viongozi wao wamekula fedha za rambirambi zilizochangishwa katika maegesho yao.

Bodaboda hao waliandamana juzi wakiwa na jeneza lenye mwili wa mwenzao mpaka kwenye ofisi yao kuu iliyoko Mtaa wa Misheni, wakishinikiza fedha zirejeshwe na viongozi wao kujiuzulu mara moja.

Wakizungumza katika ofisi hizo, baadhi ya madereva hao wa bodaboda walidai kuwa wanachanga fedha za rambirambi kati ya Sh. milioni 2.5 hadi Sh. milioni 2.8 kila msiba unapotokea lakini wakati wa maziko zimekuwa zikitolewa Sh. 800,000 na kwamba hali hiyo imewachosha.

"Fedha hizi tunazichanga waendesha bodaboda wa halmashauri nzima na kiwango chetu ni zaidi ya Sh. milioni 2.8 lakini cha kushangaza tunaletewa 800,000 kwa ajili ya kuendeshea msiba wa mwenzetu tunataka kujua fedha zingine wanapeleka wapi?" alihoji Selemani Mwakyembe, mmoja wa waendesha bodaboda hao.

"Wametuchangisha pesa zetu wakituharakisha ili wapeleke msibani, lakini mpaka wakati huu hata wafiwa hawajapata hata mia," aliongeza.

Dereva mwingine wa bodaboda, Hamis Joseph, alisema katiba ya umoja wao inawataka viongozi kushika nafasi kwa miaka mitatu, lakini hao wameng'ang'ania kwa miaka saba sasa.

Juhudi za kuwapata viongozi hao ziligonga mwamba baada kudaiwa kuzikimbia ofisi zao.

Aliyekuwa Katibu wa Umoja huo, Fred Fideli, alisema umoja wao una zaidi ya wanachama 2,000 na kwamba wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku.

Fideli alisema jukumu la kila mwanachama ni kuchangia fedha za rambirambi kwa mujibu wa sheria zao.

Alisema linapojitokeza tatizo kama hilo, viongozi wao wanatakiwa kujibu kiasi kilichopatikana, tumika na kubaki ili kuondoa sintofahamu miongoni mwao.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Geita, Manjale Magambo, alifika katika ofisi za umoja huo kutuliza vurugu huku akitoa Sh. 500,000 kwa ajili ya kuwawezesha bodaboda hao kumaliza msiba huo.

Aliahidi kufanya kikao kikubwa leo kusikiliza kero zao na kupata ufafanuzi kutoka kwa viongozi hao ili kuondoa migogoro baina yao mara kwa mara.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Geita, lilifika eneo la tukio hilo na kuwasihi bodaboda hao kuwa watulivu wakati suala lao linashughulikiwa.



Mwendesha pikipiki akiwa ameshehеni mizigo na abiria akiwa amesimama katika eneo la Msongola, jijini Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ajali treni, gari magereza yaua askari, yajeruhi

**Na Beatrice Shayo**

ASKARI wa Magereza, Twaibu Sultan, amefariki dunia na watu 10 kujeruhiwa wakiwamo askari wanane na mfungwa baada ya basi la magereza kugonga treni ya abiria katika eneo la Ukonga, jijini Dar es Salaam.

Askari aliyefariki dunia ni dereva wa basi hilo lenye namba MT 0040 mali ya Jeshi la Magereza lililogonga treni ya abiria namba YD16 yenye injini namba 9015 iliyokuwa inatokea mikoa ya bara (Morogoro, Dodoma, Tabora na Kigoma).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk, ajali hiyo imetokea juzi saa 11:23 jioni.

Alisema basi la magereza lilikuwa na watu 15 na wakati ajali hiyo ikitokea lilikuwa likivuka reli eneo la kilometa 13 Ukonga na ndipo lilipogonga treni iliyokuwa na abiria 650.

"Ajali hiyo imesababisha kifo cha mtu mmoja na majeruhi 10 ambao ni wanawake watano na wanaume watano. Majeruhi walipelekwa Hospitali ya Rufani ya Amana kwa ajili ya matibabu,"alisema.

Mbarouk alisema shirika linaendelea kuwasihi madereva wa vyombo vya moto kuwa makini wanapokatiza reli kwa kufuata sheria na alama za usalama wa reli zilizowekwa ili kuepusha ajali.

"Shirika linatoa pole kwa ndugu wa marehemu na Mwenyezi Mungu awape nafuu majeruhi ili waweze kuendelea na shughuli za kujenga taifa,".

Jana, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka, aliwatembelea majeruhi waliolazwa Taasisi ya Tiba na Mifupa (MOI).

Alisema anasikitika kutangaza kifo cha askari wake mmoja na kutoa pole kwa majeruhi.

Jenerali Nyamka amewataka madereva wote wa Jeshi la Magereza kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisitokee.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Jeshi la Magereza, Juma Kapilima, alisema askari nane wamejeruhiwa na mfungwa mmoja ambao walipatiwa matibabu na wengine kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Alisema katika Hospitali ya Amana yupo Ofisa mmoja na MOI yupo mfungwa akiendelea na matibabu.

# EWURA yafungia vituo madai kuficha mafuta

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imesema imevifungia vituo saba vya mafuta nchini kutoa huduma kwa madai ya kuficha mafuta kwa lengo la kujipatia faida kinyume na sheria.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Titus Kaguo, alisema jana mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua zilizochukuliwa dhidi ya vituo hivyo baada ya kubainika kuwa vilificha mafuta na kusababisha uhaba wa bidhaa hiyo nchini.

Alisema kuanzia Julai, mwaka huu, kumekuwapo na matukio kwa baadhi ya maeneo ya pembezoni mwa nchi kukosa mafuta hasa kipindi bei zinapoelekea kubadilishwa na kusababisha usumbufu kwa wananchi na athari za kiuchumi.

Alisema baada ya malalamiko hayo, EWURA ilifanya uchunguzi na kubaini kuna vituo vya mafuta nchini vilikuwa vikificha nishati hiyo ili kujipatia faida bei inapopandishwa na mamlaka hiyo.

"Pamoja na mafuta kuwapo nchini upungufu wa mafuta katika maeneo mbalimbali ulichangiwa na baadhi ya wamiliki wa vituo vya kuuzia mafuta kwa makusudi kuamua kuhodhi mafuta, " alisema Kaguo.

Alisema EWURA imeendelea kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kuvifungia vituo vinavyothibitika kuficha mafuta kinyume na kanuni na miongozo inayosimamia biashara ya mafuta nchini.

"Kama tulivyoeleza katika mkutano na waandishi wa habari tarehe 18 mwezi huu kule Dar es Saalam EWURA iliendelea na uchunguzi wa vituo vingine ikiwemo kupata fursa ya kuwasilisha utetezi wao ndani ya siku 21," alisema.

Alisema baada ya kupitia utetezi wao katika kikao cha Septemba, mwaka huu, Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA ilijiridhisha pasipo shaka kuwa vituo viwili vilitenda kosa la kuhodhi mafuta kati ya Julai na Agosti na kuamuru vifungiwe kwa kipindi cha miezi sita.

Alivitaja vituo hivyo kuwa ni Rashal Petroleum Ltd cha Mlimba mkoani Morogoro na Kimashuku Investment Co. Ltd cha Babati mkoani Manyara.

"EWURA inatoa onyo kwa wamiliki wa vituo vya mafuta kuwa serikali inafuatilia suala hili kwa karibu kupitia vyombo vyake mbalimbali na kuwa ikidhibitika uvunjaji wa sheria na kanuni umetendeka hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwemo kuwafutia leseni zao," alisisitiza.

**LOSS OF CERTIFICATE OF INCORPORATION NO: 3999**

**I, CHARLES BENEDICT MBERESERO** being the Chairperson of the Registered Trustees of **ALLI MBERESERO FOUNDATION,** Do hereby announce the loss of the original Certificate for Incorporation of Registered Trustees of **ALLI MBERESERO FOUNDATION.** The Certificate was lost on 05th Day of September, 2023. The information for the loss has been reported to the police. **(PHQ/KIL/MWA/2336/2023.**

**KIWANJA KINAUZWA**

Kiwanja kizuri kilichopo ITV Mikocheni chenye sq.m 4,560, karibu na benki ya CRDB Mikocheni Branch na Nyumba za Mawaziri kinauzwa.

Kinafaa kwa kupaki malori, Yard ya Ujenzi, Jengo la Ofisi, Kiwanda nk.

**Simu 0716 266525.**

# Bashungwa akerwa kasi ujenzi uwanja wa ndege

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameelezea kukerwa na kasi ndogo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, hivyo kuiagiza kampuni ya Beijing Construction Engineering Group kukamilisha ujenzi wa jengo la abiria na la kuongozea ndege ifikapo Desemba, 2024.

Bashungwa alisema hayo juzi jijini Dodoma wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanja hicho na kutokuridhishwa na kasi ya maendeleo yake kutokana na kusuasua kwa mkandarasi huyo.

"Mkandarasi usivimbe kichwa kana kwamba umepata kazi nyingi. Usipozingatia maelekezo ambayo nimekupatia, kulingana na vipengele vilivyopo kwenye mkataba, tunaweza kukusimamisha kazi kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alimtahadharisha mkandarasi huyo iwapo atazembea kukamilisha kazi hiyo kwa wakati hatapata kazi nyingine katika sekta ya ujenzi ndani ya nchi.

"Ukizembea kwenye kazi hizi, nina mamalaka ya kuhakikisha hupati kazi nyingine ndani ya nchi hii, baada ya ziara hii nataka kuona kazi inaenda kwa spidi," alisisitiza Bashungwa.

Aidha, Bashungwa amemtaka Meneja Mkazi wa Kampuni hiyo, kuripoti ofisini kwake na kumwandikia maelezo ya mpango kazi wake na 'kuweka kwa maandishi namna atakavyokamilisha mradi huo kwa wakati.

Pia alimwelekeza msimamizi wa miradi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kusimamia mradi huo saa 24 ili ukamilike kwa ubora na kwa wakati kama ilivyopangwa.

Bashungwa alibainisha kuwa ujenzi wa jengo hilo unatekelezwa kwa awamu mbili na kwamba sehemu ya kwanza inahusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua kwa ndege yenye urefu wa kilomita 3.6, maegesho ya ndege, njia ya magari barabara za maingilio na hadi sasa utekelezaji wake ni asilimia 36.

Sehemu ya pili inahusisha ujenzi wa jengo la abiria pamoja na jengo la kuongozea ndege na miundombinu mingine ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 7.

Awali wakati akikagua barababara ya kuruka na kutua ndege, Bashungwa alimpongeza mkandarasi Sinohydro Corporation anayeshirikiana na M/s Beijing Sino - Aero Construction Engineering na M/s China Jiangxi International Economic and Technical Cooperation kwa kuendelea kutekeleza mradi huo na kumsisitiza kuendelea kufanya kazi usiku na mchana ili uweze kumalizika kwa wakati.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Mohamed Besta, alisema watahakikisha wanawasimamia makandarasi wote wawili wanaojenga kiwanja hicho ili kumalizika ndani ya muda kwa kuweka sawa ratiba yao ili iendane na muda waliopangiwa na kupata matokeo wanayoyatarajia.

Ukamilikaji wa kiwanja hicho ambacho sehemu ya kwanza ya ujenzi wake inagharimu Sh. bilioni 165 ni moja ya mkakati wa serikali katika kuboresha na kuimarisha usafiri wa anga, ambapo kiwanja hicho kitakuwa na uwezo wa kupokea abiria milioni 1.5 kwa mwaka na abiria 800 kwa wakati mmoja.



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Florian Mtey (wa pili kushoto), akipata maelezo kuhusu namna ya kupika supu ya pweza kutoka kwa Bakari Kanducha (kushoto) kutoka Chuo cha National Of Tanzania, katika maonyesho ya vyakula vya asili kwa kanda zote za Tanzania, jijini Dar es Salaam juzi. Wa (tatu kushoto) ni Kaimu Makamu wa Chuo Utalii, Jesca William. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CHADEMA yaibua hoja kuhusu uboreshaji daftari wapigakura

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeiomba serikali kutoa ratiba ya uboreshaji daftari la wapigakura kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika (pichani), alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusu masuala mbalimbali yanayoendelea nchini.

Mnyika alisema serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa kutoa ratiba ya uboreshaji wa daftari hilo ambalo kiutaratibu linatakiwa kuboreshwa mara mbili kabla ya kufanyika uchaguzi za rais, wabunge na madiwani mwaka 2025.

"Ukiangalia hadi sasa mwaka 2023 daftari hili lilipaswa kuwa tayari limefanyiwa maboresho, hivyo basi natoa wito kwa serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Tume ya Uchaguzi (NEC) kutoa ratiba ili kuanza kuboresha daftari hili la wapiga kura kwa mujibu wa utaratibu,"alisisitiza Mnyika

Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliboresha daftari hilo mwaka 2017/18 na kutumika katika uchaguzi mkuu uliofanyika nchini mwaka 2020.



Awali aliitaka serikali kuacha kujimilikisha mchakato wa kuandaa sera ya elimu na mitaala mipya ya elimu kwa kuwashirikisha wadau wote kwa maslahi ya taifa.

"Siyo sawa serikali ikajimilikisha zoezi hili na mchakato wa upatikanaji wa sera mpya na mitaala mipya ya elimu nchini," alisema na kuongeza:

"Mjadala wa elimu haupaswi kujadiliwa na kuridhiwa na serikali peke yake mapendekezo yaliyotolewa kuhusu mitaala na sera ya elimu hayajajitosheleza katika kuvusha nchi yetu kwenda mbele."

Alisema serikali inatakiwa kupata mapendekezo ya kuboresha mfumo wa elimu nchini kutoka katika makundi yote kwa kuwa watu wote watakwenda kunufaika na maboresho hayo bila kujali chama.

"Mitaala hiyo haitakuwa ya chama kimoja bali itakwenda kugusa Watanzania wote wanafunzi wa sasa na watoto wa watoto wetu, ni lazima watu wote tushiriki kuamua hatma ya jambo hili kwa pamoja bila kumwacha mtu nyuma," alisema.

Alisema kwa namna ambavyo mchakato huo umeendeshwa hadi ulipofikia, wao kama CHADEMA hawajaridhishwa na mapendekezo yaliyotolewa kwani bado yanahitaji kuboreshwa ili kupata mfumo wa elimu ulio bora na shindani na mataifa mengine.

Kadhalika, alisema serikali inaandaa dira ya taifa ya mwaka 2050 ambayo hawajashirikishwa.

"Haiwezekani chama kimoja kuandaa dira ya taifa hadi mwaka 2050 bila sisi kushirikishwa, dira ni ya miaka mingi ambayo kama sisi tukiingia madarakani tutatakiwa kuitekeleza lakini leo hii hatushiriki katika kuiandaa, haiwezekani hata kama hatupo serikalini lazima uwepo mlango wa sisi kushiriki kuandaa jambo hili, " alisema.

Aliitaka serikali itoe kauli ya kuelekeza mchakato mzima wa uandishi wa dira ya taifa kwa makundi mengine.

"Serikali pamoja na kuzindua mchakato huu bado haijaelekeza namna ambavyo makundi mengine yaliyo nje ya serikali ya CCM (Chama cha Mapinduzi) yanaweza kushiriki hatua kwa hatua kuandaa dira hii ya taifa ya mwaka 2050," alisema.

HABARI KITAIFA

# Kasi magonjwa ya moyo yamnyima usingizi Waziri

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kasi ya ongezeko la magonjwa ya moyo, hususan shinikizo la damu ni moja ya mambo ambayo yanamnyima usingizi, hivyo kuna haja ya kila Mtanzania kutafakari kuhusu afya ya moyo ambayo ndiyo kitovu cha uhai.

Aidha, amewataka Watanzania kubadilisha mfumo wa maisha ya kisasa wa kutumia vitu vyenye sukari nyingi, mafuta na sigara aina ya shisha na kujikita katika ulaji wa matunda na mboga za majani ili kuimarisha afya.

Ummy aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani iliyofanyika katika Hospitali ya Dar Group - JKCI ambayo yalikwenda sambamba na utoaji wa huduma za uchunguzi na matibabu bure ya moyo kwa wananchi.

Alisema utafiti umebaini ni asilimia tatu pekee ya Watanzania watu wazima, ndio hula matunda na mboga za majani, hali ambayo alisema inahatarisha afya, hivyo ili kuepukana na magonjwa ya moyo ni wakati wa kubadili dhana zinazohatarisha afya kwa ulaji usiozingatia lishe.

"Matibabu ya moyo ni ghali sana hadi kufikia Sh. milioni 10 kufanya upasuaji wa kubadilisha valvu kwenye moyo iwapo moyo wako mishipa imeleta shida.

"Tanzania hatuna shida ya upatikanaji mboga, hivyo tule mboga. Wataalamu watuelimishe namna ya kupika hizi mboga kwani tunaivisha sana, si sahihi. Kule kwetu Tanga, Dar es Salaam mboga inawekwa viungo vingi. Pia tuzingatie kufanya mazoezi dakika 150 kwa wiki," alisema.

Ummya alisema wataalamu wanashuhudia kasi ya ongezeko la wagonjwa wa moyo Tanzania. Alisema mwaka 2017 kulikuwa wagonjwa milioni 2.5 na mwaka jana walifikia milioni 3.4, huku wengi wakiugua shinikizo la damu.

Alisema magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu ndiyo yana kasi kubwa kutoka asilimia moja mwaka 1980 hadi asilimia tisa mwaka 2020. Alisisitiza wanaougua hasa shinikizo la damu kutumia dawa ili kuepukana na magonjwa ya moyo kama kisukari, figo na kiharusi.

"Katika kila Watanzania 100 wenye miaka kuanzia 15 na kuendelea, 12 wana presha (shinikizo la damu). Mei, mwaka huu, nilitoa taarifa kuhusu presha na ndiyo sababu ya changamoto ya magonjwa haya. Ukijulikana mapema ni rahisi kutibu ugonjwa, tujitokeze kupima afya," alisema Ummy.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Angela Muhozya, alisema matatizo ya moyo yanaongezeka kwa asilimia 25 kila mwezi na kati ya wote wanaofika kwa ajili ya uchunguzi katika taasisi hiyo, asilimia 35 hadi 50 hukutwa na matatizo ya moyo.

"Ndani ya robo mwaka tunahudumia wagonjwa 2,000 ikiwamo tawi letu lililopo Hospitali ya Dar Group JKCI. Idara ya dharura tunaona zaidi ya wagonjwa 500 kwa robo mwaka Dar Group JKCI.

"Kasi ya magonjwa ya moyo inaongezeka, hivyo kuna haja ya kuongeza kasi ya kutoa elimu katika jamii ikiwa ni pamoja na kuwafikia wananchi pale walipo kupitia TibaMkoba," alisema Dk. Muhozya.

Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Moyo Tanzania (TCS), Dk. Robert Mvungi, alisema kati ya vifo vyote vitokanavyo na magonjwa tofauti nchini, asilimia 13 chanzo ni magonjwa ya moyo.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Islamic Help, Mohasaad Mohammed (katikati), akimtwisha ndoo ya maji kichwani mwanafunzi wa kidato cha kwanza wa Shule ya Sekondari ya Chatuu, Asia Kivumbi wakati wa uzinduzi wa kisima cha maji chenye thamani ya sh. milioni 16 kilichochimbwa na taasisi hiyo kwa ufadhili wa watu wa Kuwait, wilayani Muheza mkoani Tanga hivi karibuni. Kulia ni Diwani wa kata ya Mtindiro, Mustafa Hatibu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Taasisi zatakiwa kukuza sekta ya madini

**Pilly Kigome na Alphonce Kabilondo,** GEITA

SERIKALI imesema sekta ya madini ni lazima iungane na nyingine nchini ili ikue haraka kiuchumi na kuongeza ajira kwa wananchi.

Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Dk. Hemed Suileman Abdulla, wakati akifunga maonyesho ya sita ya teknolojia ya madini katika viwanja vya Bombambili mkoani hapa.

Dk. Hemed alisema sekta hiyo ya madini inatakiwa kuungana na ya elimu, fedha na sayansi na teknolojia kwani ni muhimu kuiendeleza kwa kuwa inatajwa kuleta maendeleo endelevu nchini.

Mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 7.3 kwa mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 9.1 mwaka 2022.

Mafanikio hayo, alisema yametokana na maboresho yaliyofanywa katika usimamizi wa sekta na kuweka mazingira wezeshi ya biashara.

Alisema sekta hiyo imeongeza mchango katika ajira kwa wananchi kupata moja kwa moja kwenye madini na kandarasi zinazotolewa na migodi. Alisema hadi sasa migodi yote mikubwa na ya kati inatumia huduma zinazotolewa na Watanzania.

Alibainisha kuwa tayari mitambo mitatu ya usafishaji wa madini na fedha imejengwa katika mikoa ya Dodoma, Mwanza na Geita ikiwa na uwezo wa kusafisha kilo 965 kwa siku.

Mitambo hiyo, alisema ina uwezo wa kusafisha kwa asilimia 99.99 dhahabu na fedha.

" Jambo ambalo litaiwezesha nchi yetu kupitia Benki Kuu ya Tanzania kununua madini na kuyahifadhi ili kuimarisha shilingi ya Tanzania," alisema na kusisitiza:

"Natoa wito kwa Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kuweka akiba ya dhahabu ya kutosha, pia wachimbaji wadogo na wakubwa kutumia mitambo hiyo ya usafishaji wa madini ili kupunguza upotevu wa mapato yatokanayo na kuuza madini yasiyosafishwa."

Waziri wa Madini, Antony Mavunde, aliitaka sekta hiyo kuchangia pato la Taifa hadi kufikia asilimia kumi ifikapo mwaka 2025 kutoka asilimia 9.1 ya mwaka huu.

Mavunde alisema maonyesho hayo yameendelea kukua kwani washiriki wameweza kupata elimu ikiwemo ya matumizi sahihi ya teknolojia na uhifadhi wa mazingira.

Alisema sekta hiyo imezidi kukua na inachangia pato la Taifa kwa asilimia 56 kwa fedha za kigeni.

Mavunde alisema wizara hiyo inakusudia kufanya utafiti wa kijiolojia nchi nzima kwa kutumia ndege lengo ikiwa ni kuhakikisha wachimbaji wanaondokana na uchimbaji wa kubahatisha.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella, akitoa taarifa kuhusu maonyesho hayo, alisema yatakuwa yanafanyika kila mwaka. Alisema katika maonyesho ya mwaka huu, washiriki wameongezeka hadi kufikia 350 kutoka 250 mwaka jana.

Alisema baadhi ya washiriki hao ni makampuni na wajasiriamali kutoka ndani na nje ya nchi, ikiwemo Burundi, Kenya, Uganda na Rwanda.

# Sera, usimamizi wa fedha yaleta matokeo chanya

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, amesema kuwapo kwa sera nzuri, usimamizi wa fedha na uwezeshaji katika kilimo kumeleta matokeo chanya kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa zinazozalishwa na wakulima wadogo na wa kati.

Alisema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati akifunga warsha ya siku moja iliyokuwa ikijadili namna bora ya kuwekeza katika sekta ya kilimo kwa maendeleo endelevu ya taifa.

Warsha hiyo iliandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya kuwainua wakulima wadogo kiuchumi (MEDA) iliyokuwa na lengo la kuwakutanisha pamoja wadau wa kilimo nchini.

Dk. Hashil alisema warsha hiyo ni matokeo ya mkutano wa kimataifa wa masuala ya kilimo uliofanyika Dar es Salaam hivi karibuni chini ya usimamizi na uongozi imara wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Naipongeza taasisi isiyo ya kiserikali ya kuwainua wakulima wadogo kiuchumi kwa kuwakutanisha pamoja wadau wa kilimo nchini katika warsha hii iliyokuwa na majadiliano ya namna bora ya kuwekeza katika sekta ya kilimo kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu," alisema.

Mwakilishi Mkaazi wa Taasisi hiyo, Mussa Lubango, alisema lengo kuu la kuwapo kwa warsha hiyo ni kuwainua wakulima wadogo na wa kati katika sekta ya uchumi na maendeleo endelevu.

Vile vile, kuwapo muunganiko kama huo utatoa fursa ya masoko kwa wawekezaji katika kuzalisha mazao mbalimbali ya kibiashara na chakula nchini.

"Pongezi kwa serikali kupitia kwa wizara husika kwa kutupa ushirikiano mzuri na kuwezesha warsha hii kufanyika nchini kwani tunaiona Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula katika ukanda wa Afrika na Mashariki ya Kati," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Simbachawene iwafumbue iwageuze kifikra viongozi serikalini

**WAZIRI** wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, juzi alikuwa akifungua programu ya uongozi ngazi ya cheti awamu ya nne iliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi. Mafunzo hayo yana lengo la kuwanoa watumishi hao kwa ajili ya kufanya kazi kwa tija na ufanisi na watakaposhika nafasi za uongozi, watende mambo kwa weledi.

Katika hotuba yake, Simbachawene alikemea tabia ya baadhi ya watumishi waandamizi wa umma na viongozi katika wizara, taasisi na idara serikalini, kujifanya miungu watu huku wengine wakiwatisha watu kwa kusema 'unajua mimi ni nani? Kwa maneno mengine watu hao hutumia nafasi zao vibaya kwa kuwanyanyasa watu walio chini yao na wananchi kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Simbachawene, baadhi ya watu hao wanapopata nafasi za uongozi, badala ya kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa utumishi wa umma, hufanya mambo yao ikiwamo kuwahamisha watu wanaowakuta na kuwapachika watu wao ili kutimiza maslahi yao binafsi. Viongozi hao, alisema wamekuwa wakifanya hivyo kwa visingizio kwamba hawaendani na kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Kutokana na kukithiri kwa tabia hiyo, aliwakumbusha viongozi wa umma katika ngazi mbalimbali kuacha ubabe na umungu mtu bali watekeleze majukumu yao kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizowekwa katika utumishi wa umma.

Aliwakumbusha pia wanaopatiwa mafunzo ya uongozi kwamba watakapohitimu wakatekeleze majukumu yao kwa misingi hiyo.

Simbachawene hakuishia kutoa nasaha hizo pekee bali aliweka wazi kwamba mtu anapopewa nafasi ya uongozi, anapaswa kuwa na maono ili kuleta tija na matokeo chanya katika sekta anayoiongoza badala ya kuwa mtu wa kupiga watu, kulipiza visasi na kufanya ukatili wa aina mbalimbali.

Pia alisema kiongozi anapaswa kuwabadilisha kifikra wale anaowaongoza na kuwashirikisha katika kuyatafsiri maono aliyo nayo na hatimaye kuifikia njozi iliyotarajiwa.

Waswahili wana msemo kwamba "Kisu kimegonga mfupa". Kauli hiyo ya Waziri Simbachawene imewagusa viongozi na maofisa wengi katika utumishi wa umma ambao wameendeleza umangimeza, umungu mtu, visasi na unyanyasaji. Viongozi na maofisa hao, pindi wanapopata nafasi, hutumia kama fimbo kuwapigia wengine huku wengine wakisema "sasa watanitambua".


Viongozi wanapaswa kutambua kwamba dhamana wanayopewa si kwa manufaa yao bali ni kuwatumikia watu. Kwa kushindwa kutambua hilo, ndiyo maana katika ngazi mbalimbali za utumishi wa umma, rushwa na kauli za njoo kesho, zimetamalaki. Pia wako ambao wameshindwa kujiamini katika nafasi zao, hivyo kuona watu wenye uwezo lakini wako chini yao wanawadharau. Hatua hiyo imesababisha badala ya kutoa maagizo kwa wasaidizi wao, hutumia kauli ya 'maagizo kutoka juu'.

Ni wakati mwafaka sasa kwa viongozi wa serikali na taasisi zake kutambua kuwa uongozi ni kuongozwa na watu kwa maana ya kufuata ushauri mzuri ili kutekeleza yanayopaswa kufanywa. Pia watambue kuwa matendo ndiyo yatakayodhihirishwa na watu wanaowaongoza kwa kutenda matendo mema.

Yako mambo mengi ambayo kiongozi anatakiwa kufanya kwa manufaa ya jamii anayoiongoza badala ya kujitutumua na kunyanyasa watu. Kwa maneno mengine, mtu anapopewa nafasi ya uongozi anapaswa kufanya mambo ambayo hata akiondoka jamii itamkumbuka na kuwa alama ya ukumbusho.

Ni vyema viongozi walioko katika nafasi mbalimbali, ziwe za umma au taasisi binafsi, kujifunza kupitia kauli ya Waziri Simbachawene kwamba waache kujiona miungu watu na kutaka kuwanyanyasa watu kwa kutumia nafasi zao. Kwa kufanya hivyo, maendeleo endelevu yatapatikana na kero zinazowakabili wananchi zitapungua kwa kiasi kikubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vijana kataeni kuwa chawa kwa maslahi ya watu binafsi



Na Sabato Kasika

**HIVI** karibuni, umeibuka mtindo wa baadhi ya vijana ambao ni mashabiki wa vyama vya siasa kuwa sehemu ya kubeba maslahi ya watu binafsi ambao wamepachikwa jina la 'chawa', linalozidi kuwa maarufu.

Uchawa huo ni kwamba vijana wanageuka kuwa wafuasi wa mtu badala ya kubeba maono ya chama, kitendo ambacho kiongozi huyo akiondoka, wanaweza kujikuta hawana mahali pa kuegemea.

Ninadhani kuna haja ya vijana kubadilika na kuepuka kutumika badala yake wajipange kutafuta nafasi mbalimbali za uongozi katika vyama vyao badala ya kutumika kwa maslahi ya watu binafsi.

Mtindo huo wa uchawa umemkera pia Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, ambaye aliwahi kuwaambia vijana wa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM) kuwa waachane nao wasimamie maslahi ya chama.

Chongolo alitoa onyo hilo wakati akihutubia wajumbe wa Baraza Kuu la UVCCM hivi karibuni na kusema CCM inategemea vijana hao kutumia nafasi zao kubeba ajenda za chama zenye maslahi kwa taifa.

Aliwataka wasikubali kuwa sehemu ya kubeba maslahi binafsi ya watu wachache wenye ndoto zinazokinzana na misingi ya chama, hivyo wazingatie maslahi ya umma wa Watanzania.

Kwa mujibu wa Chongolo, chama kinawategemea vijana wa jumuiya hiyo ili kukilinda na kukisemea na kufanya mambo yatakayokifanya kiendelee kuwa chama tawala nchini na si vinginevyo.

Msisitizo wake ni kwamba vijana wasiache wajibu huo, wasiache kulinda viongozi wao, wasibebe jukumu la kuwa viongozi wa watu na kwamba kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha majukumu yao.

Aliwataka vijana kusimama na viongozi halali na sahihi wa taasisi na sio viongozi wanaojiandaa kuwa viongozi bila kuandaliwa na taasisi, kwa maelezo kwamba, viongozi wengi wanaojiandaa na kuwa na tamaa ya nafasi, kwenye chama hicho, huwa hawapati nafasi.

Ninaunga mkono kauli ya Chongolo kwani ni wazi kwamba kijana akiamua kuwa mfuasi wa mtu badala ya chama, mtu huyo akiondoka au akishindwa, anaweza kujikuta katika wakati mgumu kwa kutengwa.

Ingekuwa vyema kama vijana wataacha tabia ya uchawa na badala yake wajifunze kujipigania na kujisimamia wenyewe ili kufikia malengo waliyojiwekea katika maisha yao.

Si siri kwamba njia rahisi ambayo baadhi ya vijana wameigundua kwa sasa ni kuwa chawa, ambayo sidhani kama ni sahihi, kwani inalenga kushabikia au kubeba maslahi ya watu wachache badala ya taasisi.

Kwa muda mrefu vijana wamekuwa wakitumika kwa maslahi binafsi ya wanasiasa, wakati mwingine katika uchaguzi huwa wanatumika kufanya vurugu au kupigana na wenzao wa vyama vingine.

Sasa limekuja jina la uchawa ambalo wahusika ni wale wanaoshabikia maslahi ya watu wachache badala ya chama, na wanaweza kujikuta wakiingizwa katika mtego wa kushiriki vurugu kwa maslahi binafsi.

Hivyo ingekuwa ni vyema kama onyo lililotolewa na Changolo likaleta matokeo chanya ili kuepusha kuingia katika mtego ambao mwisho wao unaweza usiwe mzuri kwa kutumiwa na kuachwa walivyo.

Kifupi ni kwamba vijana wasikubali kutumiwa na wanasiasa, kwani wakishawatumia na kupata kile wanachokitaka wanawaacha kama walivyo na kuendelea kuwa chawa huku wakiacha fursa za kuwaletea maendeleo.

Ni muhimu vijana wajipiganie kwani ni wengi na wana uwezo wa kufanyiana kampeni na kuwania nafasi nyingi za uongozi na kuibuka na ushindi badala ya kuwa wasindikizaji kwa mtindo wa uchawa.

Wakumbuke kwamba, wanasiasa wakishamaliza kuwatumia, hawana haja nao tena, hivyo wasikubali kuwa nyuma ya wanasiasa na kuwasafishia njia bali wachangamkie fursa mbalimbali za uongozi.

## FIKRA MBADALA

# Mtu akipewa heshima, ajiheshimu



Pascal Mayalla

LEO naendelea na makala elimishi kuhusu hadhi ya ubalozi nikianza kwa pongezi kwa mmoja wa mabalozi wapya walioteuliwa hivi karibuni, akiwamo John Ulanga, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Wiki iliyopita tuliishia katika kipengele nani anaweza kuwa Balozi na ana hadhi gani. Leo nazungumzia mambo kadhaa, kwanza, haki za mtu mwenye hadhi ya ubalozi. Haki na hadhi za kibalozi ziko nyingi zikiwamo wenza wa watu wenye nafasi hiyo kupatiwa pasipoti za kidiplomasia, wenza kulipiwa posho pamoja na watoto wao wasiozidi wanne na kulipiwa ada katika shule za kimataifa.

Eneo la ubalozi na nyumba za wanadiplomasia vinahesabika ni nchi husika, hivyo vina kinga ya kidiplomasia. Polisi haruhusiwi kuingia au kukamata mtu, hivyo mhalifu yeyote au hata kibaka akifanya uhalifu na kukimbilia ubalozi wowote, hawezi kukamatwa mpaka ubalozi wenyewe umripoti na kuruhusu akamatwe.

Hii ni kama ilivyotokea kwa Jullian Asange au Tundu Lissu. Ukitafutwa na polisi ukakimbilia ubalozi wowote, polisi hawawezi kukukamata, ila watakungojea hapo nje, ukitoka tu unadakwa.

Haki nyingine ni kutembelea gari la kibalozi lenye namba za ubalozi. Balozi akiwamo ndani ya gari inapeperushwa bendera ya nchi husika. Ikitokea kuna msongamano wa magari barabarani, gari hilo linawasha taa na linapishwa kama magari ya zimamoto, kubeba wagonjwa na ving'ora.

Wanadiplomasia hasa mabalozi hawalipi kodi, wana vitambulisho maalum na wananunua bidhaa katika maduka maalum, maarufu kama 'duty free'. Mabalozi pia wanalipwa posho za kuwawezesha kuishi vizuri na kwa utulivu, hivyo mishahara yao yote huwa kama akiba tu. Kuanzia nyumba bure, usafiri bure, ada unalipiwa, wenza wanalipwa, matibabu bure, usafiri ni wa daraja la biashara kwenye ndege na balozi daraja la kwanza. Mwenza anapewa nafasi ya upendeleo ya kuajiriwa ubalozini kama mfanyakazi mzawa.

Hata hivyo, Si kila mwanadiplomasia ubalozini ana kinga ya kidiplomasia. Kinga za kidiplomasia anapewa tu mtu mwenye hadhi ya ubalozi. Kinga hizi zina hadhi mbalimbali, ziko za wanadiplomasia wenyewe hasa maofisa ubalozi wenye hadhi za ubalozi na zingine ni maofisa ubalozi wenye hadhi zisizo na kinga ya kidiplomasia, wakiwamo wana familia, maofisa wa kawaida wenye pasipoti za kidiplomasia lakini hawana kinga.

Pamoja na kwamba kuna watu wanateuliwa kuwa mabalozi, si kila Balozi lazima awakilishe nchi. Kama nilivyosema, kuna mabalozi wa kuteuliwa na mabalozi wa kuajiriwa. Katika mabalozi wa kuajiriwa, mtu anaweza kupanda cheo hadi kufikia ngazi ya Balozi lakini akaishia kuwa ofisa wa kawaida katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kuna baadhi ya nafasi ili mtu ashike lazima awe na hadhi ya ubalozi zikiwamo Katibu Mkuu Kiongozi, Mkuu wa Chuo cha Diplomasia, au Mkurugenzi wa Idara katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika mashariki.

**KUPOTEZA UBALOZI**

Ubalozi ni hadhi ya heshima sana. Mtu anapoteuliwa kuiwakilisha nchi kama Balozi lazima awe mwadilifu na mwenye kujiheshimu. Asiwe mlevi, mropokaji na awe nadhifu muda wote kiakili na kimtazamo ndiyo maana mabalozi wanalipwa posho za mavazi. Maofisa ubalozi wote wanatakiwa wasifanye makosa ya jinai na kuzingatia miiko ya kinga za kidiplomasia.

Mkataba wa Vienna (Vienna Convention) umeweka utaratibu ofisa ubalozi yeyote akitaka kufanya jambo lolote nje ya shughuli za kibalozi, lazima aandike barua ya kibalozi iitwayo 'Note Verbale' katika Wizara ya Mambo kuomba kibali na kujibiwa ndipo afanye hivyo.

Jambo lingine, kila mwanadiplomasia anayefanya jinai ni lazima avuliwe Ubalozi. Kuna jinai za aina mbili, ya kwanza ni jinai katika utekelezaji wa majukumu na ya pili ni ya binafsi. Mwanadiplomasia akifanya jinai katika kutekeleza wajibu wake, nchi husika ama inamfukuza na kumrejesha nyumbani. Lakini akifanya jinai binafsi kama vile ulevi, kusababisha ajali au kuua, anapaswa avuliwe hadhi ya ubalozi na sheria za nchi husika kuchukua mkondo wake.

Lakini kwa maofisa ubalozi wa nchi za kimagharibi kama Marekani, ofisa wake wa ubalozi popote akifanya jinai, nchi yake inakinga na kumwondosha haraka kurejea. Akifika tu anavuliwa ubalozi mara moja na kustaafishwa. Nchi husika ikimhitaji kuja kujibu tuhuma, wanasema alishastaafu na hawajui habari zake ili kumkinga dhidi ya kesi.

**MIZIGO YA KIDIPLOMASIA**

Hii ni mizigo ya ubalozi ambayo huingizwa na kutolewa bila kukaguliwa kwa kuwa ina kinga za kidiplomasia. Rais wa nchi anaposafiri, pia mizigo yote ya msafara wake inapewa hadhi ya kidiplomasia, hakuna kodi wala ukaguzi. Serikali za wasio waaminifu huutumia mwanya huu kubeba mambo yao.

Pamoja na hayo, si watu wote ni wanadiplomasia lakini kwa nafasi zao wanapata hadhi ya kidiplomasia. Mfano wabunge wana pasipoti za kidiplomasia lakini si mabalozi. Wakuu wa taasisi za kimataifa na kitaifa pia wana pasipoti za kidiplomasia.

Aidha, baadhi ya wafanyabiashara wakubwa pia wana pasipoti za kidiplomasia. Lengo la kuwa na pasi hizo za kusafiria ni kuwawezesha kupita sehemu kwa urahisi kulingana na hadhi zao.

Mtu mwenye hadhi ya kibalozi, kama maisha yake aliyaendesha kwa kutegemea hadhi hiyo, kitendo cha kuvuliwa, hatua ya kwanza ni kupokwa pasipoti ya kidiplomasia. Kwa hiyo mfumo wake wa maisha unabadilika mara moja. Kama ni dukani anapanga foleni kama wengine. Hakuna watumishi wa kukubebea mizigo yako.

Kinachofuatia ni athari za kisaikolojia na kama hajajiandaa, anaweza kukumbwa na sonona na msongo wa mawazo. Lakini hili si kwa watu wenye misimamo kama alivyo Dk. Willibrod Slaa. Huyu ni mtu anayetoka katika eneo la watu wenye uvumilivu mkubwa na anaweza kuishi maisha ya aina yoyote.

Mwandishi ni mwanahabari aliyefanya kazi ubalozini kwa miaka minne kama mfanyakazi mzawa. Ametembelea Balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali za Afrika, Ulaya, Asia na America.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tusibweteke na uenyeji AFCON tujipange sawasawa



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KWA kawaida kila mzazi humsomesha mwanawe kwa matarajio ya kupata mafanikio zaidi. Hivyo amalizapo darasa la saba, mzazi huomba sana mwanawe afanikiwe na kuendelea na sekondari.

Hata hivyo, wako wazazi ambao mafanikio ya watoto wao kielimu, huyapokea kwa hisia hasi kiasi cha kuwazuia kuendelea hata kama wamechaguliwa.

Hao ni wale wanaotarajia kuona watoto wao hususan wa kike, wakipata wachumba wa kuwaoa kwa nia ya wazazi kujipatia utajiri kutokana na mahari itakayolipwa.

Lakini wako pia wanaozuia watoto wao wa kiume kuendelea na masomo na kuwataka kubaki nyumbani wakichunga mifugo na kufanya kazi zingine za uzalishaji mali, kikiwamo kilimo.

Kwa wazazi ambao watoto wao hufanikiwa kuingia sekondari, hufanya maandalizi makubwa, kuhakikisha kuwa waliochaguliwa wanaendelea kufanya vizuri katika masomo hayo na kupanda ngazi zaidi kielimu.

Juzi, Tanzania kwa kushirikiana na Kenya na Uganda, zilichaguliwa kuwa waandaaji wa fainali za soka Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika mwaka 2027.

Katika kuonyesha furaha hiyo, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, akiwa Misri ambako mchakato wa kupata mwenyeji ulifanyika, hakujizuia kulia kwa furaha akionekana mubashara duniani.

Matokeo yaliyotangazwa na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Dk Patrice Motsepe, yalizionyesha nchi hizo tatu za ukanda unaounda Baraza la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika Mashariki (CECAFA), zikizishinda Algeria (iliyojitoa mwishoni), Misri na Botswana.

Waziri wa Utanadni, Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro, ni miongoni mwa walioshuhudia kinyang'anyiro na bila shaka alifurahi sana sambamba na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameonyesha kupenda michezo kwa kiwango cha juu, hususan soka.

Lakini pia Watanzania wote wameifurahia hatua hii, ambayo inaiingiza nchi kwenye ramani ya kimataifa kisoka, huku ikiwa pia ni fursa ya nchi kuendelea kujitangaza pia kimataifa.

Bila shaka mwaka 2027 ni wa hekaheka si tu Tanzania bali Afrika Mashariki kutokana na fainali hizo, itakuwa ni fursa nzuri kibiashara na kitalii kwa mataifa haya ndugu wa miaka mingi.

Kwa Tanzania, tusibaki kushangilia na kubweteka, ni muda mwingine wa kujipanga kimiundombinu lakini pia kiukarimu, kwani tukifanya mchezo, CAF haitasita kukatiza fursa hii na kuihamishia kwingine kutokana na uzembe wetu na mengine, kwani tunajuana.

Katika miaka hii iliyobaki mpaka kufikia muda huo, Tanzania tuhakikishe mwanetu huyu aliyefaulu kwenda sekondari, anapata maandalizi mazuri kiakili, kimwili lakini pia kimiundombinu na kivifaa, ili akafanikiwe katika masomo yake 2027.

Masomo hayo ni pamoja na kufaulu kutwaa Kombe la AFCON badala ya kuishia kuwa mwenyeji na kuliacha likienda mataifa mengine ya Afrika. Itakuwa aibu kubwa si tu kwetu, bali kwa Afrika Mashariki.

Tuhakikishe kuwa tuna timu nzuri ya taifa, kwa maana ya Taifa Stars, yenye wachezaji watakaotutoa kimasomaso katika michuano hiyo. Tunajua, wachezaji wenye umaarufu nchini kwa sasa ni wageni wanaocheza katika klabu zetu za Ligi Kuu.

Tunajua usajili wa wachezaji 12 wa kigeni katika klabu zetu hizo, unawawekea kauzibe wenyeji na baadhi yao kukata tamaa na hivyo kuishindwa kuchomoza katika michuano ya kimataifa kama hiyo.

Tulijikuta tukitoa uraia kwa wachezaji kama Kibu Dennis wa Simba, ambaye hivi sasa anakipiga na Taifa Stars, kwani kama tungekuwa na wachezaji wazuri wa kiwango chake au zaidi kusingekuwa na haja hiyo, lakini hapakuwa na jinsi.

Tukumbuke tuna wacheza wengi wazuri wazawa, lakini wanacheza Ughaibuni wakiwa na uraia wa mataifa mengine, mathalan mchezaji nguli kama Nestory Irankunda, mwenye asili ya Burundi lakini aliyezaliwa Kigoma, anayecheza sasa Ligi A ya Australia.

Ni kijana aliyezaliwa Februari 9, 2006 na sasa ni winga matata wa klabu ya Adelaide United na ambaye sasa timu ya Ligi Kuu ya Ujerumani ya Bayern Munchen inamfukuzia na alishasema yuko tayari kuichezea Taifa Stars.

Yuko pia Bernard Kamungo kiungo wa FC Dallas ya Marekani, aliyezaliwa Kasulu mkoani Kigoma Januari Mosi, 2002 na kabla akizichezea Abilene Warbirds na North Texas SC na hivi karibuni alitajwa kupambana na Lionel Messi katika mechi Marekani na kufanikiwa kupachika bao.

Wawili hawa wakichanganywa na wengine, ambao tunaambiwa wanaweza kufikia 60 ughaibuni, wanaweza kuunda timu kali ya kutwaa kombe hilo. Ni muda mwafaka sasa hadi kufikia 2027 tukafikiria tena suala la uraia pacha ili kuwapata galacha hawa wa soka.

**Kila la heri!**

# Silinde ambana mkandarasi mradi umwagiliaji

**Na Renatha Msungu**

NAIBU Waziri wa Kilimo, David Silinde, amemwagiza mkandarasi kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Shamba la Msimba la Wakala wa Mbegu za kilimo (ASA), wilayani Kilosa, Morogoro.

Silinde amemtaka mkandarasi huyo kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo kwa wakati na kuanza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji.

Silinde alitoa agizo hilo jana wakati akikagua shughuli za ASA katika shamba hilo ambalo huzalisha mbegu.

Alisema pamoja na mkandarasi huyo kufanya vizuri katika ujenzi wa mradi wa umwagiliaji shamba la mbegu Kilimi na shamba la mbegu Ngaramtoni mkoani Arusha, anapaswa kuongeza jitihada za ujenzi katika shamba hilo.

Naibu Waziri alisema Msimba ni miongoni mwa mashamba makubwa ya ASA, hivyo mkandarasi anapaswa kuongeza vifaa na wataalamu ili kazi hiyo ikamilike kwa wakati na umwagiliaji uanze haraka kama wizara inavyotaka.

Silinde pia alikagua ujenzi wa uzio wa shamba, kitalu cha miche ya michikichi na mtambo wa kuchakata mbegu.

Alimpongeza Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, na menejimenti yake kwa kufanya kazi vizuri na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za kilimo.

Dk. Kashenge alisema wamepokea maelekezo ya serikali na kuahidi kuyafanyia kazi ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea ya kuzalisha mbegu bora.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka alisema serikali ya wilaya hiyo itaendelea kutoa ushirikiano kwa ASA kuelimisha wananchi waishio pembezoni mwa shamba hilo na kulilinda.



Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile (kushoto), akimsikiliza Mkuu wa Shule ya Mafunzo ya Anga wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Denis Mwageni (kulia), alipotembelea miradi mbalimbali ya chuo hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# RPC aanika mbinu kudhibiti uhalifu

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Wilibroad Mutafungwa, amesema jeshi hilo limejipanga kuzuia matukio ya uhalifu kwa kuelimisha jamii kupitia vitengo mbalimbali kuliko kutumia nguvu kupambana na matukio hayo.

Ametoa kauli hiyo juzi wakati wa hafla ya kuwatunuku vyeti vya heshima askari 54 wa vyeo na wakaguzi waliofanya vizuri katika vitengo husika huku akiwakumbusha kuongeza juhudi katika kuimarisha ulinzi wa Watanzania.

Mutafungwa alisema kuwa, kwa sasa wameweka nguvu katika kuelimisha jamii kupitia makundi mbalimbali kuhusu kudhibiti uhalifu katika jamii zao na kupunguza matumizi makubwa ya nguvu kwa jeshi hilo.

Alisema wamekuwa wakiendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali kuanzia ngazi ya mitaa.

"Kwa sasa vitendo vya ukatili mkoani Mwanza vimepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na mwendelezo wa utolewaji wa elimu katika jamii unaofanywa na Jeshi la Polisi kupitia kitengo cha dawati la jinsia kwa kushirikiana na wadau wengine,"alisema Mutafungwa.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, ambaye amemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, alilipongeza jeshi hilo kwa mpango wao wa kuweka polisi kila Kata ambao umesaidia kwa asilimia kubwa kudhibiti uhalifu katika maeneo husika.

"Uamuzi huu ni nguzo imara katika kutokomeza uhalifu, lakini ninaomba kuwaagiza sasa mshuke kwenye jamii na kufanya upelelezi kuhusu vitendo vya ukatili na kuhakikisha vinadhibitiwa ili kuweka jamii katika hali ya usalama," alisema Makilagi.

# Uswisi kuwawezesha vijana 1,600 kujiajiri

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI ya Uswisi imetoa Sh. milioni 139 kwa ajili ya kuwapatia mafunzo vijana 1,600 wanaotoka katika familia maskini mkoani hapa ya ufundi stadi, kilimo na ufugaji ili kujiajiri na kujipatia kipato.

Fedha hizo zimetolewa na ubalozi wa Uswisi nchini kwa vijana hao wa halmashauri za wilaya za Malinyi, Kilombero, Mvomero, Gairo, Kilosa na Manispaa ya Morogoro.

Kwa mujibu wa Ofisa Mradi wa Ubalozi wa Uswisi nchini, Rasheed Mbalamula, mradi huo utatekelezwa kwa kushirikiana na serikali za wilaya ziliko halmashauri hizo kwa njia ya matamasha hayo.

Mbalamula alisema mafunzo hayo yatatolewa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji Morogoro (MVIWAMORO), Shirika la Maendeleo ya Uholanzi (SNV) na Shirika la Swisscontact.

Alisema mpango huo umelenga kupata vijana 1,600 katika wilaya hizo ambao watapata ujuzi na kuingia katika soko la ajira.

Ofisa huyo alisema uamuzi wa kuhamasisha vijana hao unatokana na kila mwaka kujitokeza fursa za ajira 900,000 kwa kundi hilo, lakini wamekuwa wakipata ajira 50,000.

Alisema kutokana na idadi kubwa ya vijana kubaki bila ajira mitaani, serikali na kampuni binafsi, wameona kuna haja kundi hilo lijikite kwenye ajira za kujitegemea na kujiajiri.

Alisema ulimwengu unabadilika kila wakati katika teknolojia na maarifa, kwa kuwa vijana ndio chachu ya uvumbuzi endelevu na mabadiliko, hivyo lazima wapewe rasilimali ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, ubalozi wa Uswisi nchini umewekeza fedha kwa ajili ya kuwapatia elimu ya ufundi stadi, kilimo na ufugaji vijana wa Tanzania kwa zaidi ya miaka mitano,

Ofisa Vijana wa Mradi wa Ujuzi kwa Ajira (SET) unaotekelezwa na Swisscontact, Paul Medeye, alisema mradi huo umekuwa ukichangia juhudi za serikali kwa vijana kujiajiri kwa kuzalisha bidhaa.

Medeye, alisema SET una lenga vijana kuanzia miaka 15 hadi 24 kuwapa ujuzi vijana hususani wa kike wa ushonaji, kilimo cha mbogamboga, ufugaji wa samaki kuku, nyuki, uchakataji wa viungo na maziwa.

# MAISHA

OKTOBA 1, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14




## Milkshake' ya parachichi

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Zingatia haya unapotafuta eneo la kujenga nyumba




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# MAVAZI KIGANJANI KWAKO

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | P | I | G | W | A |
| H | ■ | ■ | ■ | O | ■ | S |
| I | ■ | P | E | N | ■ | H |
| N | O | A | ■ | G | A | O |
| D | ■ | S | A | A | ■ | N |
| W | ■ | H | ■ | ■ | ■ | W |
| A | J | A | B | U | ■ | E |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

GOA, FAA, ADA, TAA, BWATA, FAGIO, OMBWA, OGOPA, ACHANGI, MCHANGO

## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI, LEO TUNA VIFUNGU VYA MANENO, KATIKA KILA KIFUNGU KINA MAJINA MAWILI. JE, NI MAJINA YA NINI? FUATA MAELEKEZO KUNG'AMUA MAJINA HAYO KISHA YAJAZE MBELE YAKE.

Majina ya Wanafamilia

**AAMJABBMOA** __________.__________

Majina ya Vyombo vya Usafiri

**MGIEALIR** __________.__________


Majina ya Vifaa vya Shule

**NAFPTRIAEID** __________.__________

Majina ya Mifugo

**USGUKUUNRAK** __________.__________

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

JOHN alikwenda sokoni kununua nyanya na mambo yalikuwa hivi.

John: Nyanya zinauzwa kiasi gani?

Muuzaji: Kilo shilingi 1500

Kijana: Nimeagizwa unisagie tunataka kwenda kula na chipsi nyumbani

Muuzaji: Kijana usitanie kazi za watu

Swali
Chaza inapatikana sehemu gani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mahausigeli wanapoendewa kwa waganga wasiache kazi!

KARIBU msomaji wangu, naamini u mzima wa afya. Naam. Wiki moja iliyopita niliahidi kukuletea sehemu ya pili kuhusu mahausigeli tunaowaleta majumbani mwetu kufanya kazi. Wengine kumbe huendewa kwa mganga ili wasiache kazi?

Baada ya kusoma makala ile, binti mmoja amenitumia kisa chake jinsi kazi hiyo ilivyotesa maisha yake. Tulia msikilize.

Amenitumia kisa hiki kupitia Email yangu; fwingia@gmail.com, akisema hivi:-

"Habari dada, kwa kweli umenigusa sana ulivyosema kwa habari ya ukali wa kinamama kwa wasichana wao wa kazi. Ngoja nikueleze kisa changu wakati nilipokuwa hausigeli kwenye nyumba moja, japo nilifanya kazi kwenye nyumba nyingi lakini hii ilizidi Flora.

Tajiri hakuwahi kunilipa hata siku moja, japo nilimwambia asinilipe kwa kipindi kile kwa sababu nilikuwa nasoma English course kwa miezi mitatu mpaka nitakapomaliza ndio aanze kunilipa. Lakini hata nilipomaliza miezi mitatu hakunilipa hiyo miezi niliyoendelea kukaa naye.

Anti, wapo kinamama huwaendea wasichana wao wa kazi kwa mganga ili wakae nao muda mrefu wapate sifa.

Kumbe wasichana wanavumilia mateso tu, wakitaka kuondoka wanaahirisha kumbe ni nguvu za giza.

Nilikaa na mama huyu, kwanza nilikuwa nikipika chakula ananiambia nile chakula cha jana yake wao wanakula fresh nilichopika mimi na hata kama nikila kiporo kile kikabaki ni lazima nikimalizie usiku.

Mume wake akitoka safari mimi ndio nimpokee, nimwandalie maji ya kuoga nimpelekee bafuni, akitoka kuoga mimi ndio nimwandalie chakula mezani.

Kisha kumbuka chakula hicho nimepika mimi mwenyewe, mimi ndio nafua nguo za mume wake na za familia nzima. Wakati mwingine ananiambia nikatandike kitanda chake. Dada nakueleza hivi siongezi wala sipunguzi.

Ikafika mahali akawa anakuja kulala chumbani kwangu nilikuwa nalala na watoto wake, kumbe nikilala ananipaka dawa nikiwa usingizini. Siku moja nikaota nanawishwa uso, kushtuka nakuta kama nina vumbi usoni.

Nikamwona mama akawa anajifanya kama anaumwa tumbo, nikawa nimepata shaka fulani naye akahama saa ile ile kwenda chumbani kwake.

Ikafika mahali yule mama ananiambia nisikae ndani saa mumewe anakula. Na kibaya zaidi ikafika mahali mama huyu akadai nina uhusiano wa karibu na mume wake.

Ikabidi nimuite mama wa makamo pale mtaani nikamwambia amueleze yule mama kuwa sipendi anavyonipakazia. Basi yule mama akamweleza bayana mume wa bosi wangu, kisha yule baba akaweka kikao cha watu wanne, mimi, yule jirani, yeye na mke wake.

Tukamwita na mume wa yule jirani, tukaongea sana karibu saa sita usiku. Ikajulikana mchawi ni mama bosi wangu huyo.

Ukazuka ugomvi mkubwa sana usiku ule sitakaa nisahau maisha yangu yote. Sikuwa na mahusiano na yule baba, nilimheshimu kama baba yangu aliyenizaa.

Huyo mama alitaka kuniua kabisa lakini kumbuka nilikuwa nimeokoka haswa. Alikuwa ananitumia majini nikienda kanisani nikiombewa yanasema tumetoka kwa fulani na amesema tukuue (mimi), yakiulizwa kwa nini yanasema kwa vile mimi nina urafiki na mume wake.

Lakini nilimfuata nikamweleza kuwa nimemsamehe kwa yote aliyonitendea, na pia nikamwapia kwamba kama ni kweli mimi nilihusiana na mume wake basi nisifanikiwe.

Akanitamkia nitaendelea kuwa 'housegirl' maisha yangu yote. Mimi sikutaka kubishana naye kwa kujua kuwa Mungu ndiye mpangaji wa yote.

Kwa hiyo ndivyo ilivyokuwa kwa kipindi hicho dadangu. Kinamama wengi hawajui kusimamia nyumba zao mwisho wa siku wanashuku vitu vya uongo. Huko ni kuweweseka kusiko na manufaa kwao wanajipa mashaka ambayo hayapo". Hivi ndivyo anavyomaliza kisa chake msomaji huyu. Mpenzi msomaji, kisa hiki nilipokisoma kilinivutia sana.

Binti huyu amesema ukweli hadharani kuonyesha vituko vya waajiri kwa mahausigeli. Yaani mbali na kuwakopa mishahara, kumbe huwazubaisha kwa ushirikina.

Binti huyu alikuwa na Roho wa Mungu aliyemfunua kubaini mbinu chafu za mama tajiri yake kumfanyia uchawi wakati amelala. Wapo watu wanaoteseka lakini wanashindwa kujinasua.

Hata hivyo, njia pekee ya kujiondoa ni kuvunja ukimya kama alivyofanya binti huyu ili jamii ijue kuwa mahausigeli wengi tunaowaona, wengine wako vifungoni.

Wengine wakifunguka huamua kuondoka kwa mikwara kwa kuiba, kutesa watoto na kutimka zao.

Mpenzi msomaji, hiyo ndiyo hali halisi ya nyumba zetu.

***Hadi wiki ijayo. Una maoni au kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Malalamiko udanganyifu mizani yafike mwisho

UKIWASIKILIZA madereva hasa wa malori makubwa, madogo na mabasi yaendayo mikoani kuhusu makosa yanayojitokeza wakati wa kupima uzito kwenye mizani, utagundua wana hoja nzito.

Wanalalamika kwamba makosa mengi hawajui yanatokana na nini kwa kuwa kituo kimoja alichokipita, mizani ilionyesha hakuzidisha uzito wa mzigo.

Lakini katika kituo kilichofuata, alibainika amezidisha uzito. Swali je, mizani yetu inayomilikiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ni timilifu?

Inakuwaje kama ukipita mizani yetu uko sawa, kwenye baadhi ya mizani na baadhi ya mizani mzigo hauko sawa? Kama ndivyo ukivuka mpaka kwenda nje ya nchi mbona hatusikii hayo matatizo?

Labda niwakumbushe tu kwamba Tanzania tunatumia aina tatu za mifumo ya ukokotoaji uzito wa magari makubwa nchini. Mifumo ya upimaji uzito tuliyo nayo na inayotumika hivi sasa ni ile ya Data Bridge, Smart Scale na Tload.

Niwakumbushe serikali, na hasa TANROADS kwamba tunapotaka kufanana na nchi zilizoendelea kiteknolojia, ni lazima tuyaishi na kujifunza juu ya hatua walizopitia kufikia mafanikio hayo.

Nimeisoma kwa kina ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu makosa katika utozaji wa faini za kuzidisha uzito wa mizigo katika mizani inayomilikiwa na TANROADS.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA, CAG amesema baada ya kufanya mapitio ya faini za kuzidisha uzito wa upakiaji mizigo zilizotolewa na TANROADS katika mizani 13 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Amebaini magari 11,594 yalitozwa faini pungufu ya kiasi kilichotakiwa kutozwa, kwa jumla ya dola za Marekani 466,449.

Aidha, magari 134 yalitozwa faini zaidi ya kiwango kilichotakiwa, kwa jumla ya dola za Marekani 10,958, kinyume cha aya ya 11 ya jedwali namba tatu la udhibiti wa uzito wa magari wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

CAG ameeleza kuwa utozaji wa faini kinyume na taratibu unaweza kusababisha upotevu wa mapato na athari za kisheria kwa kutofuata kanuni, jambo ambalo linaweza kuharibu sifa na hadhi yake.

Kuhusu miamala isiyosuluhishwa katika taarifa za mifumo ya ankara na mfumo wa GePG (Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni),

CAG anasema katika idadi ya miamala 682, tofauti iliyobainika ni ankara zenye viwango vilivyolipwa kwa ziada (overpaid) kwenye mfumo wa data bridge,

Ukilinganisha na taarifa za malipo za mfumo wa GePG ni Sh. 16,601,526.20, na katika miamala 487, tofauti iliyobainika ni ankara zenye viwango vilivyolipwa pungufu (underpaid) kwenye mfumo wa Databridge, ukilinganisha na taarifa za malipo za mfumo wa GePG ni Sh. 7,557,402.86.

Kutokana na makosa hayo, CAG amependekeza TANROADS ifanye mapitio na kusahihisha kanuni ya mfumo inayokokotoa uzito wa ekseli na uzito wa magari ili kuhakikisha utozaji viwango sahihi vya faini za uzidishaji uzito, kwa mujibu wa udhibiti wa uzito wa magari wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kuhusu kutokuwianisha kwa mifumo TANROADS, CAG amebaini mambo kadhaa yanayohusiana na uwianishaji wa mifumo tumizi kwa TANROADS. Amebainisha kuwa ameeleza kuwa TANROADS inatumia mifumo mitatu tofauti ya mizani, ambayo ni Data Bridge, Smart Scale na Tload, kwa madhumuni sawa ya upimaji.

Zaidi ya hayo, amebaini ni mizani 13 pekee, kati ya 63 imeunganishwa kwenye seva kuu, akisisitiza hali hiyo inaleta hatari ya udanganyifu kutokana na ufuatiliaji usiotosheleza.

Aidha, ni vyema serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na TANROADS zikatoa pia elimu kuhusu faini za Wakala huyo kwa makosa ya barabarani.

Hivi ni wangapi wanaojua kuwa kwa mujibu wa Sheria ya TANROADS ya Mwaka 2007, kwamba wanayo mamlaka ya kisheria ya kukamata na kuadhibu wanaokosa kwa kuzidisha mwendo kasi barabarani?

Ni wangapi wanaojua leo kwamba ukiegesha gari vibaya barabarani, TANROADS wanayo mamlaka ya kisheria kukamata na kupiga faini?

Wengi wanadhani kwamba hiyo ni kazi ya askari wa kikosi cha usalama barabarani peke yake, la hasha. Hawaingiliani kabisa.

Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009, inawapa TANROADS, uwezo wa kukamata gari au mtu yeyote anayeharibu barabara na kumlipisha faini.

Kwamba TANROADS wanaweza kukukamata kwa overspeed (mwendo kasi), kupaki gari sehemu isiyoruhusiwa, kutiririsha mafuta, au kingine chochote kwenye sheria yao. Na wao hawaingiliani na Polisi, sana sana Polisi wanaweza kukukabidhi TANROADS.

Sheria ya Barabara, inawapa TANROADS mamlaka ya kukutoza faini ya Sh. 200,000 kwa kosa la kuzidisha mwendo (section 32 (1) & 3); 1,000,000 kutanua au kuendesha kwenye njia za waenda kwa miguu (section 49(1) (a); na 200,000 kwa wrong parking (kuegesha gari vibaya) kwa mujibu wa kanuni ya 56.


Wao kule faini yao ya chini ni Sh. 50,000. Ndugu yangu, usishangae siku moja ukikamatwa na TANROADS na kupigwa faini hizo.

***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# HARUSI




NI WIKI YA FURAHA KWA FAMILIA YA SALUM KALYANYE NA JACKLINE AMBAO BAADA YA WIKI ILIYOPITA KUSHUHUDIA NDOA YA WAPENDWA WAO, SASA NI ZAMU YA KUWAPONGEZA MAHARUSI HAO KATIKA SHEREHE YA AINA YAKE ILIYOFANYIKA UKUMBI WA MSASANI TOWER. WANANDOA HAO WANAISHI OHIO NCHINI MAREKANI.





# MITINDO



## MAVAZI KIGANJANI KWAKO

UNAAMBIWA sasa dunia imewekwa kiganjani, kila kitu unachotamani kupitia kiganja chako cha mkono pekee unaweza kukipata na kwa muda mfupi.

Hata kwenye sekta ya mitindo hali imebadilika kiasi kwamba kwa muda wa saa moja tu, unapata vazi unalolipenda tena kwa gharama nafuu tofauti na zamani.

Kutokana na mambo yote kuangaziwa katika mitandao ya kijamii, sasa unaweza kupata chaguo sahihi la mavazi kwa kuperuzi katika simu yako janja na hivyo kuacha kwenda kuhangaika madukani.

Kwa kutumia simu unaweza kuchagua na kisha kufikishiwa hadi sehemu uliko kabla ya kutakiwa kulipa.

Pamoja na teknolojia ya mawasiliano kurahisisha manunuzi, kuna mambo tofauti unatakiwa kufuata ili kuondokana na kupata bidhaa feki.

Unatakiwa kuwa makini na kampuni au mtu unayetaka kufanya naye biashara ya nguo, jihakikishie kama unamuamini au la.


Angalia kwa makini aina ya nguo unayotaka kuinunua, wakati mwingine 'iscrinshoti' ili kukupatia uhakika ndiyo uliyoiona mtandaoni.

Chunguza kwa makini nguo unayotaka kuinunua kama ina ubora na imara. Baadhi ya wauzaji wa mitandaoni wanauza bidhaa zisizo na ubora unaokubalika na kulazimika kuwa na nguo isiyodumu muda mrefu.

Angalia bei kama ina tofauti na dukani, kama ipo sawa unashauriwa kwenda mwenyewe kwenye maduka kuchagua kwani huko ni sehemu salama zaidi kwa kupata bidhaa bora.







URUMBO

Na Mary Geofrey

# Mwarubaini wa sugu katika magoti

WEUSI kwenye ngozi ya magoti na viwiko vya mikono ni jambo linawakera wanawake wengi.

Unaweza kung'arisha ngozi ya kwenye magoti na nyuma ya mikono kwa kutumia dawa asilia.

Mafuta ya mzeituni na sukari

Chukua vijiko vikubwa vinne vya mafuta ya mzaituni kisha changanya na kijiko kikubwa cha sukari kimoja halafu tumia kupaka kwenye magoti au nyuma ya mikono.

Kisha tumia kuchua kwa muda wa dakika tatu mpaka tano, kaa kwa muda wa dakika thelathini halafu nawa kwa maji ya uvuguvugu.

Utafanya hivyo mara mbili kwa siku asubuhi na jioni kwa muda wa mwezi mmoja.

**Juisi ya Alovera**

Paka juisi ya rozera iliyosagwa kwenye ngozi ya goti halafu iache kwa muda wa nusu saa kisha safisha kwa maji ya moto au vuguvugu.

Utafanya hivi kwa mara mbili kwa siku asubuhi na jioni hadi ngozi yako itakapo anza kung'aa.

Binzari manjano, asali na maziwa

Chukua binzari ya manjano kijiko kimoja kikubwa, asali vijiko vinne vya chakula na maziwa vijiko vinne vikubwa vya chakula.

Vichanganye vyote kwa pamoja kisha tumia kupaka kwenye magoti, iache kwa muda wa dakika thelathini na nawa kwa maji ya uvuguvugu.

Utafanya hivyo mara mbili kwa siku asubuhi na jioni hadi utakapo pata matokeo utakayo ridhika nayo


**Ndimu**

Kata kipande cha ndimu kisha tumia kusugua kwenye magoti.

Goti moja kwa kila kipande. Sugua kwa muda wa dakika tatu hadi tano kisha kaa nayo kwa muda wa lisaa limoja.

Utafanya hivyo mara mbili kwa siku asubuhi na jioni hadi utakapo pata matokeo utakayo ridhika nayo.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kunywa 'Milkshake' ya parachichi

PARACHICHI ni moja ya tunda linalopendwa na watu wengi na huliwa kama kisindikiza mlo wowote au kiburudisho nyakati za mchana au jioni.

Tunda hilo pia hutumiwa kutengeneza saladi, kupamba sahani na kutengeneza aina mbalimbali za juisi ya milkshake ya parachichi inayotengenezwa kwa kuchanganywa na maziwa.

Mbali na parachichi maziwa ambayo yanatumiwa katika kinywaji hiki yana faida nyingi katika mwili wa binadamu ikiwamo kuimarisha afya ya mifupa.

Kutokana na faida hizo kuna kila sababu ya kujifunza kuandaa kinywaji hiki kwa ajili yako, familia au hata wateja unaowahudumia.

Maandalizi

Tofauti na aina nyingine za juisi, milkshake ya parachichi huandaliwa kwa muda mfupi usiozidi dakika 10 ikiwa unatengeneza juisi ya kunywa watu wawili au watatu.

Hatua ya kwanza ya maandalizi ni kuchemsha maziwa ya ng'ombe, na ikiwa utatumia maziwa ya boksi ya kununua dukani basi haina haja ya kuchemsha.

Kama hautumii maziwa ya ng'ombe hiyo siyo sababu ya kushindwa kutengeneza kinywaji hiki, unaweza kuweka maziwa ya soya au korosho.

Maziwa ya soya na korosho hupatikana madukani, ila unaweza kutengeneza nyumbani kwa kuziloweka kwa saa 12 au zaidi kisha kuzisaga pamoja na maji.

Ukimaliza kuchemsha maziwa anza kuandaa maparachichi kwa kuyamenya na kuyakata vipande vidogo, kisha mimina kwenye blenda pamoja na maziwa.

Baada ya hapo saga kwa pamoja kwa muda wa dakika mbili au tatu kisha utaangalia kama mchanganyiko wako umesagika vizuri na kuwa laini.

Kumbuka 'milkshake' haichujwi hivyo saga kwa muda mrefu iwezekanavyo ili kupata mchanganyiko unaoweza kuunywa bila kuchuja.

Ongeza sukari kiasi au asali kama unapendelea kisha milkshake yako itakuwa tayari kwa kunywa.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Zingatia haya unapotafuta eneo la kujenga nyumba

KUTAFUTA ardhi ni hatua ya awali ambayo mtu hufanya katika kuelekea kujenga nyumba ya ndoto yake bila kujali mahali alipoipata ardhi hiyo.

Mtaalamu wa ujenzi, Tamiko Hatula, anasema unapochagua eneo la kujenga, yako baadhi ya mambo ambayo unapaswa kuyazingatia.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa historia ya eneo husika unalotaka kununua, kuangalia ufikikaji wake.

"Kiwanja chenye barabara pande zote huhusiana na furaha, afya njema na mafanikio, huwa na hewa, mwanga na nafasi ya kutosha. Kwa kiwanja kisichokuwa na barabara pande zote ni muhimu kuwe na barabara upande wa Kaskazini au Mashariki ili nyumba ikijengwa iwe na mwanga na hewa ya kutosha kuanzia asubuhi," anasema.

Jambo lingine ambalo anashauri kuzingatia wakati wa kutafuta kiwanja kwa ajili ya ujenzi ni pamoja na kuhakikisha eneo unalonunua ni kwa ajili ya makazi au biashara na makazi.

"Hii itakusaidia uepukane na usumbufu wa kubomolewa au kuwa na hofu ya kuhamishwa, hakikisha unafuata taratibu zote za umiliki wa ardhi zilizowekwa," anasisitiza.

Anashauri kuepuka kununua kiwanja kinachouzwa na mtu aliyepatwa na dhiki au kufilisika kwa kuwa baadae kinachangia kukukosesha furaha na amani.

Pia anashauri kuepuka kiwanja kilicho jirani au kinachopakana na maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya kijamii ikiwamo kumbi za starehe, kanisa, msikiti, kiwanda, chuo, jeshini, shule, soko, sehemu ya stendi za magari.

"Maeneo haya huwa na kelele nyingi na mara nyingi matumizi yake huathiri maeneo yaliyo jirani, ikiwamo kubadilishwa kwa matumizi wakati wowote na pia ni vigumu kulea watoto na kuwakuza kimaadili katika maeneo hayo," anadokeza.

Mengine anayoshauri kuzingatia ni kuepuka kununua eneo linalomilikiwa au lililomilikiwa na taasisi za kiimani, kuepuka eneo lililo jirani na sehemu ya taka, lenye magofu mengi, mapingamizi, chenye nyufa na mipasuko pamoja na chenye udongo wa mfinyanzi.

# Chumba cha kulala kinahitaji mambo haya

**Na Restuta James**

NI Jumapili nyingine ambayo Nipashe inakuletea maarifa ya namna ya kuifurahia nyumba yako.

Chumba cha kulala ni eneo muhimu linalohitaji kumtuliza mtu na kazi za kutwa, hivyo ni busara kutengeneza mazingira ya kuhakikisha unapata pumziko zuri wakati wa usiku.

**1. KITANDA, MASHUKA NA MITO**

Kimsingi hivi ndivyo vinavyofanya chumba kiitwe cha kulala maana ni wazi huwezi kukuta kitanda jikoni. Wataalamu wa mapambo wanashauri kuwa kamwe usikurupuke kitanda ukakiacha kikiwa rafu bila kutandika.

Wanasema kukiacha hivyo kutakupa uvivu wa kukiweka vizuri wakati wa kulala usiku kwa kuwa unaweza kurudi ukiwa umechoka.

Mito mingi inavutia kitandani hasa kama unalala peke yako. Pia rangi za mashuka ziwe tulivu lakini zisiwe za giza japokuwa sio lazima ziwe nyeupe.

**2. ZULIA**

Kama huwezi kununua linalotosha chumba kizima, ni vyema ukaweka dogo ili unapoamka miguu yako isikanyage moja kwa moja sakafu ya baridi. Pia linasaidia kukupa nafasi ya kuomba ukiwa umepiga magoti, tofauti na sakafu ambayo inakuwa ya baridi.

**3. TAA YA KIVULI**

Taa hii inatumika kama pambo linaloamua kiasi cha mwanga unachohitaji pale unapohitaji kusoma au kufanya kitu kisichohitaji mwanga mwingi.

**4. SOFA**

Ni muhimu kuwa na sehemu ya kukaa chumbani kwa ajili ya mazungumzo au kusoma. Eneo hili linasaidia kuweka matandiko pindi unapotandika kitanda.

**5. PICHA, SAA**

Picha ya kuchora inapendeza zaidi chumbani. Inaweza kuwekwa kwenye ukuta unaotazamwa na mtu aliyelala kitandani. Pia ukuta huu unaweza kuwekwa saa japokuwa wengine hupendelea kuweka saa juu ya droo za pembeni ya kitanda.


**6. PAZIA**

Chumba cha kulala kinahitaji faragha na hisia za giza hata kama kimenakshiwa kwa rangi za mwanga. Pazia sahihi zitakamilisha faragha.

**Tuwasiliane katika 0753333330.**



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
'MSOBEMSOBE' YAMETIMIA KUTINGA MAKUNDI KIMATAIFA!
JUKWAANI
ULIYEKUJA KUMKAMATA UNAMJUA AU UNAJISHAUA KUTAKA SIFA!
ALIYEKUJA KUKUKAMATA UNAMJUA AU 'UNAJIPAISHA' KUTAKA KIKI?
BABA BILA WEWE, MIMI SITOBOI
'MGAWO'
MKIAMBIWA TUNZENI VYANZO VYA MAJI NYIE WABISHI
LOH!
NIMEIKUTA MIKUBWA MIZIMA INAKOGA KWENYE MABWAWA WANA-MWAGA MIMAJI HOVYO!
TUVITUNZE KAMA MWALI MKOLENI AU TUVIBEBE?
MAJI YAME-KAUKA JUA KALI MSIWE KAMA HAMNA AKILI!
USITUTUKANE BHANA! KAMA GIZA TUNAKAA WOTE...
MBONA WAIFU UNANIBASHIRIA MABAYA KILA KUNAPOKUCHA!
UTAJUA TU KAMA 'MAFAO' NA MIONDOKO YA KUKESHA BAR NI MARAFIKI
HA HA HAAA UNAPENDWA SANA KARIBU NA KAMPENI HUJIVUNGI KUTOA HELA TUNAZILA HA HAAAAA!
NKICHEKA MIMI USIJE UKANUNA! WE HAYA
RUDIA MARA YA MWISHO NENO KIPIMO CHA KOMPYUTA
'KIPIMO CHA KONTYUPA' KULE KIJIJINI HAKUNA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
UMEPIKIA MAJI YA BAHARI CHUMVI YA NINI...

HABARI KIMATAIFA

# Russia kuitambulisha mikoa mipya

**MOSCOW,** RUSSIA

NAIBU wa Baraza la Usalama la Russia, Dmitry Medvedev amesema idadi ya maeneo mapya ya nchi hiyo itaongezeka katika siku zijazo.

Medvedev alichapisha taarifa kwenye mtandao wa telegramu yake katika hafla ya siku ya kuunganishwa tena kwa mikoa mipya kuwa maeneo mapya ya nchi hiyo na yatalindwa.

Siku hiyo ilitangazwa hivi karibuni kuwa ya mapumziko na amri ya Rais Vladimir Putin ilisema inaadhimishwa kila Septemba 30.

Aliahidi kwamba operesheni hiyo maalum ya kijeshi itaendelea hadi uharibifu kamili wa utawala wa Nazi wa Ukraine na ukombozi wa maeneo ya awali ya Russia yatoke kwa adui.

"Kutakuwa na maeneo mapya zaidi ndani ya Russia," alisema Medvedev.

Mnamo Septemba 30, 2022, viongozi wa Russia walikamilisha mchakato huo, ambao waliita kuingia kwenye shirikisho la Russia kwa mikoa minne ya Ukraine.

Ukraine na nchi nyingi ulimwengu zililitaja jaribio hilo kuwa haramu ni sawa na unyakuzi.

Uamuzi wa Russia kujumuisha mikoa minne ya Ukraine Donetsk, Luhansk, Kherson na Zaporozhye hautambuliwi na mataifa mengi, na pia ulilaaniwa na uamuzi wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Jeshi la Russia halidhibiti sehemu yote ya mikoa hiyo minne ikiwa ni pamoja na miji ya Kherson na Zaporozhye.

Ukraine ilisisitiza kuwa mazungumzo ya amani na Russia yanaweza kuanza baada ya majeshi yaliyovamia kuondolewa kabisa katika eneo linalotambulika kimataifa kuwa la Ukraine.

**BBC**



Papa Francis akiwasimika makardinali wapya katika kanisa la Mt. Peter Basilica mjini Vatcan jana. **PICHA:AP**

# Papa Francis awasimika makardinali 21 wapya

**VATCAN,** ROMA

MAPADRE 21 wa Kikatoliki walioteliwa cheo cha kardinali wamesimi kwa rasmi jana kutumikia nafasi hiyo na Kiongozi wa Kanisa hilo Papa Francis.

Makardinali hao wapya walisimikwa katika mkutano wa kawaida wa Baraza la Makardinali unaofanyika mjini Vatican.

Mnamo tarehe 9 Julai, Papa Francis aliwateua Makardinali wapya 21 kati yao watatu wanatoka bara la Afrika ambao ni Askofu mkuu mwandamizi Protase Rugambwa wa Jimbo kuu la Tabora, Tanzania, Askofu mkuu Stephen Ameyu Martin MULLA, Jimbo kuu la Juba, Sudan ya Kusini na Askofu mkuu Stephen Brislin wa Jimbo kuu la Cape Town, Afrika Kusini.

Makardinali wapya wataingizwa kwenye Jimbo kuu la Roma kama ishara ya kuonyesha mshikamano na umoja na Khalifa wa Mtakatifu Petro.

Papa Francisko alimteua Askofu Rugambwa mnamo Aprili 13, 2023 kuwa askofu mkuu mwandamizi mwenye haki ya kurithi Jimbo kuu la Tabora.

Awali alikuwa Katibu wa Baraza la Kipapa la Uinjilishaji wa Watu, huduma aliyobobea kuanzia 2002 hadi 2008.

**BBC**

# Nyangumi agonga boti, aua mmoja Australia

**DYDNEY,** AUSTRALIA

SAMAKI aina ya nyangumi ameigonga mashua nchini Australia na kumuua mtu mmoja na mwingine kupata majeraha.

Katika taarifa ya polisi ilielezwa watu hao walikuwa kwenye msafara wa uvuvi wakati mashua yao ilipogongwa karibu na La Perouse, kilomita 14 kusini-mashariki mwa mji mkuu wa Sydney.

Maofisa waligundua kuwa kuliwekwa hali ya tahadhari baada ya kuonekana chombo kikielea bila mtu yeyote na kuzunguka majini. Vifo vinavyosababishwa na nyangumi katika eneo hilo ni nadra kutokea, na waziri wa serikali wa New South Wales aliita ni ajali mbaya.

Polisi walisema katika taarifa hiyo kuwa uwezekano wa mgongano ulisababisha mashua kuinama, na kuwatupa watu wote baharini.

"Taarifa zilizopatikana mapema ni kwamba nyangumi anaweza kuvunja akiwa karibu na boti, au kwenye mashua," Kaimu Mratibu wa Polisi wa Maji, Siobhan Munro alisema.

Aliongeza kuwa hajawahi kuona tukio kama hilo kutokea huko nyuma.

Mtu aliyefariki mwenye miaka 61, alipatikana akiwa amepoteza fahamu na alipoteza maisha katika eneo la tukio kabla ya kupelekwa hospitali.

**BBC**

# Marekani yaionya Serbia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeitaka serikali ya Serbia kuwaondoa wanajeshi wake katika eneo la mpaka wake na Kosovo.

Serbia imetakiwa kuwaondoa wanajeshi wake katika eneo la mpaka wake na Kosovo, baada ya kubainika kile kilichoelezwa kuwa ni mkusanyiko mkubwa wa kijeshi.

Msemaji wa Baraza la Usalama wa taifa kwenye Ikulu ya Marekani, John Kirby aliwaambia waandishi wa habari kwamba wanafuatilia idadi kubwa ya wanajeshi wa Serbia kwenye mpaka na Kosovo.

Alitoa onyo hili baada ya Serbia kupeleka vifaru vyenye uwezo mkubwa na mizinga kwenye eneo hilo la mpaka baada ya mapigano makali kuzuka katika nyumba ya watawa kaskazini mwa Kosovo wiki iliyopita.

Katika ghasia hizo polisi mmoja wa Kosovo na washambuliaji watatu wa Serbia waliuawa, tukio hilo limechukuliwa kama moja ya kisa kibaya kutokea kwa miaka kadhaa katika eneo hilo la jimbo hilo la Kosovo lililojitenga na Serbia.

**DW**

# Watu 15 wapoteza maisha mgodini

**HARARE,** ZIMBABWE

WATU sita wamefariki dunia na wengine 15 wamekwama baada ya mgodi wa kuchimba dhahabu kuporomoka nchini Zimbabwe.

Taarifa kutoka vyombo vya habari vya nchi hiyo, inaeleza watu zaidi ya 30 walikwama ndani ya mgodi juzi asubuhi kufuatia tukio hilo la kuporomoka kwa mgodi wa dhahabu wa Bay Horse uliopo Chegutu, kilomita 100 kutoka mji mkuu Harare.

Wachimbaji 13 wanasemekana kunusurika au kuokolewa baada ya tukio hilo.

Juhudi za kuwapata wale waliokwama chini ya ardhi zinaendelea, kulingana na kituo cha televisheni cha ZBC.

Haijulikani chanzo cha kuporomoka kwa mgodi huo.

Shirikisho la Wachimbaji Madini la Zimbabwe lilisema katibu mkuu wake na mwenyekiti watakwenda kwenye eneo hilo kujaribu kubaini kilichotokea.

Ajali za uchimbaji madini nchini Zimbabwe ambayo ina akiba kubwa ya dhahabu, platinamu na almasi hazitokei mara kwa mara.

**BBC**

MAKALA

# VITABU HIVI VIAMSHE ARI YA KUJISOMEA ARUSHA DC



Na Magabilo Masambu

SERIKALI kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imetoa jumla ya vitabu 26,186 vya kiada kwa shule zote za sekondari katika halmashauri ya Arusha.

Wakati wa wa kukabidhi vitabu hivyo kwa wakuu wa shule za sekondari kwa niaba ya serikali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Selemani Msumi, alisema vitabu hivyo ni kwa ajili ya shule zote 35 za serikali huku shule tatu mpya za kata zikipokea vitabu 2,720 kwa mara ya kwanza na kufanya uwiano wa 1:1 kwa maana ya kila mwanafunzi kutumia kitabu kimoja.

Licha ya kuishukuru serikali kwa uwekezaji wa fedha nyingi katika kuboresha miundombinu ya elimu hususan shule za sekondari, Msumi alisema uwapo wa vitabu vya kutosha shuleni utarahisisha dhana ya ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia malengo ya kitaaluma yaliyo kusudiwa. Pamoja na shukrani hizo, alitoa rai kwa wakuu wa shule na walimu kusimamia utunzaji na matumizi sahihi ya vitabu si kuvifungia stoo bali kuhakikisha wanafunzi wanavitumia wakati wote wa masomo, huku kukiwa na utaratibu mzuri wa kuviazima na kuvirudisha baada ya kuvitumia.

Kuhusu mgawanyo wa vitabu hiyo, Ofisa Elimu Taaluma, Walimu Editha Chona, alisema shule tatu mpya za sekondari za kata zilizosajiliwa kati ya mwaka 2020 na 2023 zimepata vitabu 2,720 vya masomo yote. Shule hizo ni Olturoto (vitabu 873), Kiutu (1,158) Olomitu (689).

Kupatikana kwa vitebu hivyo, kumewafanya wakuu wa shule kuishukuru serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta ya elimu kwa kuhakikisha ina miundombinu ya majengo mazuri, vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na vitabu vya kiada kwa masomo yote tofauti na hapo awali.

Mwalimu Upendo Mollel, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiutu, anaesema licha ya kuwa shule yake ni mpya, kwa kipindi kifupi, serikali imewapatia vitabu 1,158 na hatua hiyo itamfanya kila mwanafunzi kutumia kitabu chake mwenyewe jambo ambalo litawaongezea uwezo ya kujifunza vizuri.

Anakiri kwamba kabla ya mgawo hu0 wa vitabu, uwiano ulikuwa ni 1:10, wakati mwingine wanafunzi walishindwa kufanya vizuri kwa kukosa vitabu vya kufanyia marejeo. Sasa uwapo wa vitabu hivyo, anasema, utawapa fursa wanafunzi kujisomea kwa nafasi na kupata maarifa hata baada ya kufundishwa na walimu darasani.

Mwalimu Jackson Mpinga, Mkuu wa Shule Sekondari Olomitu na Mkuu wa Shule ya Sekondari Olturoto, Mwalimu Peter Mlinga, kwa pamoja wanaahidi kutokomeza tatizo la upotevu wa vitabu shuleni kutokana na uzembe.

Pia wanaahidi kuandaa mpango mzuri wa utunzaji wa vitabu kwa kuanda reja ambazo zitakuwa zinatumika wakati wa kuwakabidhi mwanafunzi vitabu na kuhakikisha baada ya matumizi vinarejeshwa kwa wakati.

Ni wazi kwamba lengo la elimu si tu kuwafanya wanafunzi kufaulu mitihani yao bali elimu lazima ikusudiwe kujenga fikra za wanafunzi na fikira hizo zinapatikana vitabuni.

Vitabu hivyo vyaweza kuwa vya kiada au ziada.

Bahati mbaya tu ni kwamba utamaduni wa kusoma vitabu katika jamii yetu umekuwa chini sana, lakini ukweli ni kwamba unaposoma vitabu maana yake unazungumza moja kwa moja na waandishi wa vitabu hivyo, kwa hiyo unaweza kuzungumza na Barack Obama kupitia usomaji wa kitabu chake.

Tatizo la wanafunzi kutosoma vitabu sasa linaonekana katika uwezo wao wa kufikiri na kutenda.

Tofauti ya wanafunzi wa sasa na wale wa zamani ni katika uwezo wa kujenga hoja pamoja na uelewa wa mambo mbali mbali, wanafunzi wa zamani waliweza kuwa mahiri kutokana na usomaji wa vitabu si tu kwaajili ya kujibia mitihani.

Binafsi, kama mwandishi wa vitabu, natoa rai kwa jamii, tuwe na utamaduni wa kuwafanya watoto wetu tangu mwanzo kabisa kujenga utamaduni wa kusoma vitabu, badala ya kutumia muda mwingi kutazama picha jongefu katika runinga wakati mwingine zisizo sahihi utokana na umri wao.

Mzazi anzisha maktaba ndogo nyumbani weka vitabu mbalimbali vya hadithi nzuri, vya masomo yake shuleni, magazeti mbalimbali baada ya muda utashangaa uwezo wa mtoto wako.

Serikali inafanya upande wake kwa maana ya vitabu vya kujibia mitihani, lakini sisi kama wazazi upande wetu tuwajenge wawe mahiri. Watu maarufu wenye uwezo wa kujenga hoja ni matokeo mazuri ya usomaji wa vitabu, ukiona mwanasheria mzuri, dakitari, mwalimu, jaji nakadhalika siri yake ni kwamba wamekuwa wasomaji wazuri wa vitabu.

***0589157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***Arusha-Tanzania.***

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Nyota na mwezi usiku vinang'aa, unajua bili yake analipa nani?



Na Adam Fungamwango

UKITULIZA akili sawasawa na kuanza kuitafakari dunia ilivyo na vyote vilivyomo ndani, utagundua kuwa haviko kwa bahati mbaya. Utagundua vimepangwa kwa ustadi mkubwa.

Na yeyote aliye nyuma ya hili ni mwenye nguvu, uwezo mkubwa, hesabu kali, hekima na huruma pia.

Angalia wanyama na ndege. Hawalimi, hawaendi kazini, hawana pesa lakini wanakula na kuishi wakifurahia maisha. Majani yanaota kwa ajili yao. Hata wanyama wanaokula wanyama wenzao wanapata mlo kamili.

Hesabu yake au ikolojia ni kwamba wanyama wanaokula majani wanazaliwa kwa wingi kwa sababu wanatakiwa wawe chakula cha wanyama wanaokula nyama na wengine wabaki kuishi ili kuendelea kuzaliana.

Ndege nao ni hivyo hivyo. Wengine wanakula nafaka, wengine wanakula mizoga na wapo wanaokula samaki hai. Walivyoumbwa wanakuwa na midomo kikubwa iliyochongoka na uwezo wa kwenda ziwani, mtoni au baharini na kuwakamata samaki walio hai na kupata mlo.

Kinyonga aina fulani ya mijusi. Huyu anatembea taratibu sana. Atatembea kinyonge sana lakini anakula wadudu walio hai.

Hali majani, mizoga wala punje za nafaka, lakini utashangaa na ugoigoi ule anawapata vipi? Lakini ukweli ni kwamba anapata chakula chake kama kawaida kila siku. Hakuna siku anayolala njaa. Anakula kwa ulimi wake mrefu. Akiutoa tu unakwenda mbali kuwanasa wadudu walio hai, anaurudisha na kuwameza.

Ina maana na yeye amepewa uwezo wa kujipatia riziki yake. Narudia tena kusema kila kitu kinachoonekana duniani hakipo kwa bahati mbaya. Kimekaa kimkakati.

Maji yametengwa kwake na ardhi iko sehemu yake. Kuna mito, milima, majabali, tambarare, miinuko na vitu vingi vinavyofanana na hivyo. Nani amefanya yote haya?

Hapa ndipo binadamu anapokiri uwapo wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye aliyefanya yote haya.

Na wana msemo wao wanasema 'Mungu hakupi kilema anakunyima mwendo.'

Hata binadamu awe na kasoro gani, atakuwa mahiri kwa kitu kingine. Hata uwe mnyonge vipi, utapata riziki yako.

Moja ya vitu ambavyo binadamu anakiri kuwa dunia ina mwenyewe ambaye ni Mwenyezi Mungu, ni pale kila mmoja anapata riziki yake ya kila siku kwa jinsi alivyojaaliwa.

Anakiri kama riziki angekuwa anatoa binadamu mwenzake, basi kuna wengine wasingepata kwa sababu baadhi ya binadamu wana tabia ya ubinafsi, kujikweza, kupenda kunyenyekewa ili kutoa kitu, lakini pia roho mbaya tu.

Hewa ya oksijeni ambayo viumbe vyote duniani vinatakiwa kuivuta ili kuishi, vinatajwa kuwa ni uthibitisho wa dunia hii ina mwenyewe, ambaye anaitoa bure kwa viumbe wake na hakumpatia yeyote ili agawe.

Kama angepewa binadamu basi wengine wangenyimwa, wengine wasingepata.

Anajua itifaki wa binadamu kuna watu wa maana wangetakiwa kupewa kwanza, wengine wasubiri kwanza. Na wengine wangeweza kuambiwa hawana sifa za kupata hewa hiyo hapa duniani.

Watu wangebaguliwa. Wakati mwingine ingeanza kuuzwa kama vocha, au kulipia kama umeme.

Mzee mmoja wa miaka 70, alimshukuru na kumtukuza Mungu baada ya kukaa chumba cha uangalizi maalumu (ICU) hospitalini kiasi cha wiki mbili akipumulia mashine.

Alipopona alikuta deni la kiasi cha Sh. milioni 50 hivi. Akashangaa na kujiuliza kama amevuta hewa ya oksijeni kwa miaka yote 70 alitakiwa kumlipa Mungu kiasi gani?

Lakini miaka yote amekuwa akivuta bure tu.

Wakati umeme unalipiwa, mwezi na nyota ziko juu angani kwa kuwaangazia viumbe wote, lakini vyote ni bure tu. Hakuna kulipa wala bili.

Kwa kuona hivyo, bendi ya Polisi Jazz haikukaa kimya. Ikafikiri yote na kuja na kibao kinachoitwa 'Dunia' mwanzoni miaka ya 1980, utunzi wake Moshi William, kabla hajajiunga na Juwata Jazz na kupachikwa jina la TX.

*"Dunia, dunia hooohoooo, Dunia, dunia hooohoooo, misitu na milima, mabonde na mito, misitu na milima baba haa, mabonde na mito, wowo, vyote hivyo tutaviacha baba, hoowe hoowe hoowe mamaaa.*

*Nyota na mwezi mama hooo , usiku vinang'ara, nyota na mwezi baba hoo, usiku vinang'ara mama, bili yake analipa nani, hoowe analipa nani hoowe hoowe hoowe hoowe mamaaa.*

*Watu mashujaa mama ho, wanapotea, watu maarufu mama haa wanapotea haha, kweli dunia kweli dunia haha hoowe hoowe hoowe mamaaa.*

*Dunia ni watu mama dunia siyo ardhi. Ooooh Afrika wee Afrika wee Afrika we ohoho*

*Dunia ni watu mama dunia siyo ardhi. Ooooh Afrika wee Afrika wee Afrika we ohoho*

*Dunia ni watu mama dunia siyo ardhi. Ni watu we, niwatu we, ni watu ohohoo*

*Dunia ni watu mama dunia siyo ardhi. Ni watu we, niwatu we, ni watu ohohoo, mashujaa wee ohohoo."*

Hii ndiyo dunia ya Mungu. Hakuna kulipa bili ya oksijeni, nyota wala mwezi. Ametoa bure kwa waja wake.

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie kwenu-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Akishirikiana na rafiki yake mmoja Rozi, waliamua kutorosha Tabora na kwenda jijini Dar es Salaam kutafuta kazi. Kwa bahati nzuri walipata, kila mtu kwake.

Farida alipata bahati ya kupata kazi kama haugeli katika nyumba ya Joel Kamagi maeneo ya Mbezi Louis Dar es Salaam, ambaye alikuwa anajiweza kimaisha.

Alikuwa na kampuni zake mbili za kusafirisha mizigo. Alikuwa na malori matano. Pia alikuwa na kiwanda cha kufyatulia na kuuza matofali.

Alikuwa na hoteli moja maeneo ya Kisutu Dar es Salaam. Akawa na zingine ndogo ndogo. Kifupi alikuwa mfanyabiashara mkubwa.

Kamagi alikuwa na mke pamoja na watoto watatu, wa kike wawili na wa kiume mmoja ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa wanasoma mikoani wakikaa bweni, hivyo mara nyingi walikuwa hawaishi nyumbani mpaka likizo.

Farida alifanya kazi zake vizuri na kutokea kupendwa na waajiri wale. Miezi sita tu baada ya kuwa hapo alinawiri na kupendeza kiasi cha kumvutia mwanaume yoyote yule mkware.

Farida alifanya kazi zake vizuri na kutokea kupendwa na waajiri wale. Miezi sita tu baada ya kuwa hapo alinawiri na kupendeza kiasi cha kumvutia mwanaume yoyote yule mkware.

Miaka mitatu baadaye Farida alianza kubadilika. Alianza kuwa mvivu na kupenda kulala tu.

Mama mwenye nyumba alipokagua vizuri akagundua kuwa tayari ameshakuwa mjamzito.

Jambo hilo lilimshtua.

"Mimba ameipata wapi tena toba mtoto huyu wakati huwa hatoki hapa? Mbona hata sokoni anapelekwa na gari? Au dereva?" Akawaza mama mwenye nyumba.

"Atanieleza."

Siku aliyoamua kufanya hivyo ambapo hakuwepo mtu yeyote nyumbani alimwita chumbani kwake.

"Kaa hapo!" Akaambiwa kwa sauti ambayo Farida mwenyewe alijua haikuwa ya heri.

"Hebu niambie ukweli, usinifiche, wewe ni mjamzito au?"

Hakujibu chochote. Alionekana kushtushwa na swali lile.

"Si nakuuliza? Au hujasikia?"

"Nimesikia mama."

"Sasa mbona hunijibu?"

"Lakini mama..."

"Hakuna cha lakini, nataka jibu, una mimba huna?"




**"Baba alikuwa ananitishia kuwa nikisema ataniua kwa bastola. Na yeye alishawahi kunionyeshea bastoka hiyo hiyo kuwa nikisema ataniua!"**

Farida aliinama chini. Hakujua kama aseme ndiyo au hapana.

Na hakujua jibu gani kati ya hayo mawili yatakayomtoa kwenye dhahama hiyo.

"Jibu wewe." Mama mwenye nyumba hakumkumshusha kwa maneno tu, bali kwa maneno na kuchapa kofi moja la kumtisha."

Hakuonekana kutishika sana ingawa alipiga kelele kutaka asamehewe.

Monica hakuridhika. Akafunga mlango wa chumbani.

Halafu akaelekea kwenye kabati la nguo kwenye droo ya chini. Kama kuna kitu hivi alisahau. Akaelekea kwenye begi akionekana kutafuta kitu. Alipoutoa mkono wake ulikuwa umeshika funguo.

Wakati wote huo Farida alikuwa amekaa chini na kujikunyata huku machozi yakimtoka asijue la kufanya.

Akimwangalia bosi wake ambaye alionekana ni kama amepagawa hivi.

Akivuta hatua kadhaa kuelekea kule alikokwenda mwanzo kabatini. Akachomeka ufunguo kwenye droo cha chini, akaivuta.

Akaupeleka mkono wake ndani na kutoka na kitu alichoshika mkononi.

Kitu hicho kilizidi kumtisha Farida ambapo aliona sasa amekwisha. Yuko kwenda dakika chache kabla ya kuiacha dunia na kuelekea ahera.

Mama mwenye nyumba alikuwa ameshika bastola. Kwake Farida ilikuwa kama ndoto.

"Mpumbavu wewe usiponiambia nani amekupa hiyo mimba?" Akafoka mate yakimtoka kama kobra.

Farida aligaragara chini na kulia kwa sauti na kuomboleza," nitakwambia mama lakini usiniue, nisamehe siyo kosa langu."

"Nakwambia we mtoto, ukiniambia ukweli nakusamehe, lakini ukinificha au kunidanganya, nakutoa ubongo." Monica alizidi kumtisha huku akiwa ameishikilia kwa ufasaha bastola.

"Ndiyo mama nakwambia."

"Nani?"

"Baba!"

"Baba?"

"Ndiyo"

"Baba yako nani?"

"Huyu huyu wa ndani!"

"Mzee Kamagi?"

"Ndiyo mama!"

Nusura bastola imponyoke Monica! Hakuamini kama mumewe anaweza kufanya jambo kama lile kutembea na msichana wa kazi ambaye alikuja kuomba kazi akiwa ametoka Tabora vijijini akiwa hana mbele wala nyuma.

Nguvu zilimuishia. Ubongo wake haukutaka kuamini ingawa alishaanza kuhisi kitu kama hicho kwa mbali.

Kitendo cha kumtishia bastola alitaka kujua kitu asichopenda kujua.

Kwa sababu mtoto wake wa kiume anaishi bwenini, alichofikiria kama binti yule hakupachikwa mimba na dereva, basi huenda ni mumewe.

Ndiyo maana akatumia nguvu kubwa kumlazimisha Farida aseme. Lakini alitamani aseme ujauzito ulikuwa wa dereva. Wapiii! Mumewe ndiye kalizua.

Aliduwaa na kuwaza kwa dakika moja nzima! Ndipo alipogundua ana bastola mkononi ambayo inaweza kusababisha maafa kwa binti yule kama atachezesha kidole chake. Akaiweka mezani akionekana amechoka na majibu hayo.

Akakumbuka kuwa bado anatakiwa kumuuliza maswali Farida.

"Mmekuwa mkifanya ujinga huu kwa muda gani?"

"Muda mrefu mama ni mwaka mzima!"

"Kwa nini hukuniambia?" Akafoka.

"Baba alikuwa ananitishia kuwa nikisema ataniua kwa bastola. Na yeye alishawahi kunionyeshea bastoka hiyo hiyo kuwa nikisema ataniua!"

Ni kweli bastola ile ilikuwa ni ya Joel Kamagi.

Alikuwa mmiliki wa silaha hiyo kihalali kwa ajili ya kumlinda na mambo yake ya kibiashara.

Nyumba haikuwa na amani tena. Ulitokea ugomvi mkubwa wa kutishiana hata kuuana baina ya Kamagi na mkewe Monica.

Farida mwenyewe akatimuliwa na ujauzito wake, akarejea kwao Tabora kwenye kijiji cha Mtakwenda. Kwa bahati mbaya alimkuta shangazi yake ambaye alimlea baada ya kifo cha mama yake Tabu.

Alipojaribu kwenda kwa ndugu za baba yake mzee Katandukila hakupata msaada wowote kwa sababu walihofia akiishi pale anaweza kudai mali za baba yake mzazi, au kupata msaada kutoka kwa watu mbalimbali wenye huruma na wanaojua historia vizuri, hivyo kuwa hatari kwa ndugu waliodhulumu mali.

Alipoona hata kijijini kwenyewe hakueleweki akaamua kurejea Dar es Salaam.

Safari hii alifikia na kupewa hifadhi ya rafiki yake waliotoroka naye kijijini walipokuja Dar.

Mwenzake baada ya kufanya kazi miaka miwili tu alipata mchumba, akamtoa kwenye kazi na kufunga naye ndoa.

Rozi alimhudumia rafiki yake waliyetoka naye kijiji kimoja kama ndugu yake akipata sapoti kutoka kwa mumewe.

Walikuwa na roho nzuri na mume wa Rozi alimpa huduma zote kama shemeji yake, hasa baada ya kupata historia yao kuwa wote hao wawili walitoroka kijijini Tabora na kukimbilia Dar es Salaam na kupata kazi za ndani kama mahausigeli.

Siku zake zikafika, Mungu akamjalia, akajifungua mtoto wa kiume na akamwita jina la babu yake, Katandukila.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# WAANZA KUSHIKWA

## Waliosababisha kifo chake

JESHI la Polisi nchini Nigeria limethibitisha kumkamata Balogun Olamilekan Eletu, maarufu kama Sam Larry, kwa kuhusika na kifo cha mwanamuziki Ilerioluwa Aloba, aliyejulikana kwa jina la Mohbad.

Sam Larry ambaye anatoka lebo ya muziki ya Naira Maeley, amekamatwa katika uchunguzi unaoendelea kuwabaini watu waliohusika na kifo chake.

Msemaji wa Polisi, SP Benjamin Hundeyin, aliandika kwenye mtandao wa X kuwa Balogun Olamilekan Eletu yuko chini ya ulinzi wao kuanzia jana.

"Kwa sasa anasaidia uchunguzi unaoendelea." amesema

Tayari bosi wa lebo hiyo ya Marlian Record, Naira Marley, amedai kuwa anafanya mipango ya kurejea Nigeria kuheshimu wito wa polisi kufuatia uchunguzi unaoendelea kuhusu kifo hicho.

Mohbad alikufa katika mazingira ya kutatanisha mnamo Septemba 12, mwaka huu.

Katika video ambayo ilisambaa mitandaoni baada ya kifo cha mwimbaji huyo, Sam Larry alionekana akivamia kundi la muziki na kumtishia Mohbad akiwa na watu wenye silaha.



# *Hosanna ya Shekts yazidi kupaa*



MWIMBAJI wa muziki wa Injili kutoka nchini Uganda, Shekts Nelson, amewaomba mashabiki kuupokea wimbo wake mpya, Hosanna.

Akizungumza na BT, mwisho mwa wiki Shekts alisema kupitia wimbo Hosanna aliomshirikisha mrembo Same OG, amepata mashabiki wengi wapya Afrika Mashariki.

"Nimekuwa natamani kuona huduma yangu inaingia Afrika Mashariki, nashukuru Mungu kupitia Hosanna nimepata mashabiki wengi wapya hapo Tanzania," amesema Shekts ambaye ana asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ROWE KUONDOKA
KIUNGO wa kati wa Arsenal na England, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 23 anaweza kufikiria kuondoka Emirates ikiwa hatapata nafasi ya kucheza mara kwa mara kabla ya Januari. (***90min***)

### EKITIKE AWANIWA
WOLVES, West Ham, Everton na AC Milan zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Paris St-Germain Mfaransa Hugo Ekitike mwenye umri wa miaka 21. (***L'Equipe via Le10Spor***t)

### TONEY AWINDWA
NEWCASTLE United, Arsenal, Tottenham Hotspur, Manchester United na Chelsea zimenesha nia ya kumnunua Ivan Toney, ingawa Brentford wamedhamiria kukataa ombi lolote la Januari kwa mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 27. (***The Sun***)

### DIMARCO ATAKIWA
KLABU za Manchester City na Chelsea zinalenga kumnunua mlinzi wa Italia na Inter Milan, Federico Dimarco mwenye umri wa miaka 25. ***(Calciomercato)***

### MAATSEN MKATABA MPYA
CHELSEA ina matumaini kuwa mlinzi wa Uholanzi Ian Maatsen mwenye umri wa miaka 21, atasaini mkataba mpya, na mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. (***Football Insider)***

### WILLIAMS ANYATIWA
KLABU ya Brighton ina nia ya kumsajili winga wa Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21 kutoka Athletic Bilbao. ***(Fichajes)***

### VERMEEREN AFUATILIWA
KLABU nyingi zikiwemo Manchester United , Liverpool , Brighton , West Ham, Barcelona na Ajax zinafuatilia maendeleo ya kiungo wa kati wa Royal Antwerp na Ubelgiji katika kikosi cha vijana walio chini ya umri wa miaka 21, Arthur Vermeeren. (***Mundo Deportivo***)

### TAPSOBA ATAKIWA
MANCHESTER United ingependa kumsajili Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23 kama chaguo lao la kwenye orodha, pamoja na Edmond Tapsoba wa Bayer Leverkusen mwenye miaka 24. ***(Fabrizio Romano)***

### MBAPPE NA MUSTAKABALI
MMILIKI wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi amesisitiza kwamba mustakabali wa mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24 utabakia katika klabu hiyo ya Ligue 1. (***FourFourTwo)***

### MOURINHO AMTAKA DIER
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kuunganishwa tena na mlinzi wa Tottenham na England, Eric Dier huku mwenye umri wa miaka 29. ***(Mirror***)

### DE JONG MKATABA MPYA
BARCELONA wanakaribia kuongeza mkataba wa Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 26, huku kiungo huyo wa kati wa Uholanzi akilengwa na Manchester United wakati wa madirisha kadhaa ya uhamisho. (***Fichajes)***.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# ARTETA: ARSENAL IMERUHUSU MABAO MENGI ZAIDI NYUMBANI

**●●● Amesema wamekuwa wakicheza kwa hisia kupita kiasi na kuitaka timu yake....**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amebainisha kwamba, Arsenal imeruhusu mabao mengi wakiwa nyumbani kwa sababu walikuwa wanacheza kwa hisia kupita kiasi na kuitaka timu yake kuonesha utulivu zaidi katika siku zijazo.

Arsenal hawajapoteza katika mechi zao sita za mwanzo za Ligi Kuu ya England, wakishinda nne na sare mbili, na hawajaruhusu bao katika mechi zote mbili za ugenini hadi sasa, na kuandikisha ushindi wa 1-0 dhidi ya Brentford katika mechi ya raundi ya nne ya Kombe la Carabao, Jumatano.

Lakini wameruhusu mabao sita katika mechi nne za nyumbani, majuzi mara mbili wakiruhusu uongozi kutoweka katika sare ya 2-2 dhidi ya Tottenham Hotspur Jumapili iliyopita.

Alipoulizwa kama tofauti hiyo Arteta alisema: "Wakati mwingine tunakuwa na hisia kali mno. Tunataka kushambulia kwa kasi sana.

**"Hasa tukiwa nyumbani tuna makosa mengi ya mtu mmoja mmoja na hivyo ku tuletea matatizo, lakini ugenini hatujawa hivyo.**

"Ni kweli ugenini nadhani mbinu hiyo ni tofauti sana na wapinzani, lakini ni jambo ambalo tunatakiwa kuligeukia haraka kwani tukitaka uwiano wa matokeo hasa wa nyumbani ni jambo ambalo tunatakiwa kulibadilisha haraka."

Arsenal wanaruhusu wastani wa mashuti matatu yaliyolenga goli kwa kila mechi wakiwa nyumbani huku idadi hiyo ikishuka hadi asilimia 1.5 ugenini.

Zaidi ya hayo, Washibabunduki hao wameruhusu bao katika dakika ya kwanza ya mechi tatu za Ligi Kuu kwa mwaka 2023.

"Katika soka kwa ujumla, hatutabadili mtazamo wetu kuhusu jinsi tunavyotaka kushinda mpira," aliongeza Arteta.

"Na sisi ni timu yenye ukali sana na hatutabadilisha hilo.

"Inahusu kuwa na uwezo wa kubadilisha gia, hatuwezi kucheza na gia hizo wakati wote tukiwa na mpira, lazima tucheze kwa kasi tofauti na mchezo unavyohitaji hasa tukimuangalia mpinzani wetu."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
SIMBA SC
VERSUS
POWER DYNAMOS
1 | 1.30
X | 5.00
2 | 6.50

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA
MAOKOTO Deilee!
1. Wilson Vedasto - 0653 473 XXX
2. Leonard Membe - 0659 308 XXX
3. Hamisi Mbinga - 0659 884 XXX
4. Adelina Habeli - 0672 290 XXX
5. Andrea Hamisi - 0672 767 XXX
6. Rose Hamad Kitayai - 0672 776 XXX
7. Husein Husein - 0672 995 XXX
8. Nicolaus Mbaragwa - 0673 303 XXX
9. Nurdin Nurdin - 0678 411 XXX
10. Maones Chedego - 0711 910 XXX
20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ANTONY KUANZA MAZOEZI MAN UTD

**MANCHESTER,** England

WINGA wa Manchester United kutoka Brazil Antony Matheus dos Santos maarufu Antony ambaye anashutumiwa kwa unyanyasaji wa wanawake atarejea kwenye mazoezi, klabu hiyo imesema.

Antony mwenye umri wa miaka 23 amezungumza na Polisi wa Greater Manchester Septemba 28 na hakuna vikwazo vilivyowekwa kwake baada ya mahojiano hayo.

Vyanza vya habari vya United vimesema ametoa ushahidi wa kupinga vikali shutuma hizo.

Hajakamatwa au kufunguliwa mashitaka Brazil au nchini England.

Katika taarifa United imesema: "Kama mwajiri wa Antony, Manchester United imeamua kwamba atarejea kwenye mazoezi Carrington na kupatikana kwa ajili ya kucheza huku uchunguzi wa polisi ukiendelea."

Hata hivyo, Antony hakutarajiwa kwenye mazoezi na wala kwenye mchezo wa Ligi Kuu England kwenye uwanja Old Trafford kati ya Man United na Crystal Palace jana.

Hajacheza michezo minne tangu Man United ilipompatia likizo ya malipo kamili ili ashughulikie shutuma zilizotolewa na wanawake watatu tofauti akiwemo mpenzi wake wa zamani, Gabriela Cavallin.

# Chilwell aipa pigo Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino amefichua kuwa beki wa kushoto, Ben Chilwell amepata jeraha "baya" la misuli ya paja ambalo litahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Makamu nahodha huyo alichechemea katika ushindi wa 1-0 wa Chelsea dhidi ya Brighton & Hove Albion juzi , licha ya matumaini ya awali juu ya hali yake, sasa anaonekana kutarajia kuendelea kukaa nje ya uwanja.

Chelsea itamenyana na wapinzani wao Fulham katika uwanja wa Craven Cottage siku ya Jumatatu na Pochettino sasa amethibitisha kuwa Chilwell hatasafiri.

"Habari mbaya," alisema Pochettino kuhusu jeraha la Chilwell.

"Daktari aliniambia ni jeraha baya, lakini tunahitaji kutathmini siku chache zijazo."



Hata hivyo, Pochettino ana matumaini kwamba, Carney Chukwuemeka anaweza kurejea uwanjani Jumatatu baada ya kuumia, huku bosi huyo pia akisisitiza kwamba winga Noni Madueke anaweza kushiriki baada ya kushughulika na suala lake la utimamu wa mwili.

Beki wa kulia Reece James anakaribia kurejea uwanjani, lakini Pochettino alithibitisha kuwa nahodha huyo hatakuwa tayari kukabiliana na Fulham.

"Labda wiki inayofuata, tutaona," alisema Pochettino kuhusu James. "Tunahitaji kumpima, lakini tutaona."

Chelsea ilitatizika msimu uliopita wakati James na Chilwell wote wawili walikuwa nje kwa wakati mmoja, lakini Pochettino alisisitiza kuwa kikosi hicho sasa kina wachezaji wengi.

"Katika klabu zote, wachezaji muhimu huwakosa wasipocheza," alisema.

"Bila shaka huwa tunakosa wachezaji bora. Wanapokuwa katika kiwango bora, bila shaka ni baadhi ya mabeki bora zaidi wa pembeni duniani.

"Kwa nini hatukununua Ben Chilwell mwingine na Reece James mwingine? Kwa sababu kuna Reece James mmoja tu na Ben Chilwell mmoja."

Y | CHEZA USHINDE KASINO

# USHINDI 'WAMVIMBISHA KICHWA' KOCHA JKU

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa JKU, Salum Ali amesema kuwa timu yake itaendelea kufanya vizuri kwenye michezo yake ya ligi kuu Zanzibar kutokana na maandalizi yao mazuri waliyoyafanya kabla ya kuanza kwa msimu huu.

JKU juzi iliendeleza shangwe baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Maafande wenzao wa Zimamoto FC katika mzunguko wa nne wa Ligi kuu ya Zanzibar mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Mau A.

Matokeo hayo yameifanya JKU SC kufikisha pointi 10 baada ya michezo minne na kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ali alisema mwanzo mzuri alioanza nao katika Ligi Kuu ya Zanzibar ni matarajio yake kuona mwenendo huo unaendelea katika michezo ijayo kutokana na aina ya kikosi alichonacho.

"Bado Ligi mbichi sana na ngumu mno kwa sababu timu zote wachezaji wao hawajachoka na wananguvu na wanapambana sana, hivyo kupata matokeo haya ya mapema yananipa matumaini yakufikia malengo ya JKU SC, lakini pia kunawapa nguvu wachezaji kujituma zaidi ili kuendelea kupata matokeo mazuri", alisema Ali.

Aidha, alisema kuwa kikosi chake kitaendelea kujituma ili kuhakikisha wanaendeleza wimbi la ushindi kwenye ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ).

Katika michezo mingine jana, Mafunzo SC ililazimishwa suluhu na Mlandege FC mchezo uliochezwa kwenye uwanja wa Mau A, wakati Jamhuri nayo ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na Hard Rock katika Uwanja wa Finya, Kisiwani Pemba.



Washiriki wa Tamthiliya mpya ya Chanda itakayokuwa ikirushwa katika Chaneli ya Maisha Magic Bongo wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya hafla ya uzinduzi wa tamthiliya hiyo jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ni zamu ya Simba SC, Singida FG CAF

INATOKA UK. 24

aliweka wazi kikosi chake cha leo kitakuwa na mabadiliko ukilinganisha na kikosi kilichocheza mchezo wa kwanza nchini Zambia.

Mshambuliaji Jean Baleke anatarajiwa kupewa nafasi ya kuanza kutokana na mfumo ambao Robertinho anataka kuutumia leo.

Mabadiliko ya kwanza ambayo yanaweza kuonekana katika kikosi cha timu hiyo ni kwenye safu ya ulinzi ambapo Kenedy Juma anatarajiwa kuanza akicheza na Che Malone baada ya kuumia kwa Inonga.

Robertinho, aliiambia Nipashe kuwa kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo na kila kitu amekimaliza kwenye uwanja wa mazoezi kuelekea kwenye mchezo huo wa leo.

"Tunahitaji kushinda huu mchezo.., utakuwa mchezo mgumu lakini mpira kwangu ni Sanaa, sio kutumia nguvu au kusukumana, kucheza vizuri kupata matokeo mazuri na kufuzu hatua ya makundi ndio malengo yetu kwenye mchezo wa leo," alisema Robertinho.

Aidha, alisema wanawaheshimu wapinzani wao kwa kuwa ni timu nzuri na ni Mabingwa wa Zambia lakini wamejipanga vizuri kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Power Dynamos, Mwenya Chipepo alisema anafuraha kuwa Tanzania kwa mara ya pili ndani ya mwaka huu wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo.

"Tunatambua ukubwa wa Simba, haitakuwa mechi rahisi kwa sababu mechi yetu ya kwanza tulitoka sare ya mabao 2-2, vijana wangu wako tayari kuwafunga Simba nyumbani kwao," alisema Chipepo.

Alisema malengo yao makubwa ni kufuzu makundi na hawachezi kama klabu bali watacheza kupigania taifa kwa sababu wamekuja kuiwakilisha Zambia.

Simba ni timu kubwa na tumekuja hapa kuhakikisha tunamfunga Simba nyumbani kwake na kutupeleka makundi.

Katika mchezo mwingine wa timu ya Tanzania leo, wawakilishi pekee kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Singida Fountain Gate wenyewe watakuwa Misri kuumana na wenyeji wao Future FC katika kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Singida wataingia uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 walioupata kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 01/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4393 | Bologna vs Empoli | 1.66 | 3.96 | 5.15 |
| 14:00 | 5831 | Reims vs Lyon | 2.07 | 3.75 | 3.34 |
| 14:30 | 3845 | Nurnberg vs Magdeburg | 2.55 | 3.59 | 2.45 |
| 14:30 | 4932 | Union Saint Gilloise vs Charleroi | 1.56 | 4.18 | 4.87 |
| 15:00 | 3147 | Gor Mahia vs Kenya Commercial Bank | 2.14 | 2.85 | 3.56 |
| 15:00 | 3304 | Almeria vs Granada | 1.97 | 3.66 | 3.71 |
| 15:00 | 4628 | AFC Leopards vs Shabana FC | 1.73 | 3.12 | 5.01 |
| 15:00 | 5622 | Randers vs Silkeborg | 3.17 | 3.62 | 2.07 |
| 15:30 | 3148 | Sturm Graz vs WSG Wattens | 1.25 | 5.25 | 8.28 |
| 16:00 | 1954 | Sirius FK vs Degerfors | 1.57 | 3.93 | 4.54 |
| 16:00 | 1981 | Udinese vs Genoa | 2.40 | 3.14 | 3.19 |
| 16:00 | 2284 | Lillestrom vs Brann | 2.36 | 3.40 | 2.73 |
| 16:00 | 2429 | Nottingham vs Brentford | 2.78 | 3.24 | 2.62 |
| 16:00 | 2803 | Nice vs Brest | 1.78 | 3.81 | 4.43 |
| 16:00 | 2917 | Toulouse vs Metz | 2.18 | 3.44 | 3.34 |
| 16:00 | 3901 | Le Havre vs Lille | 3.81 | 3.45 | 2.01 |
| 16:00 | 4020 | Mlada Boleslav vs Bohemians | 1.96 | 3.57 | 3.47 |
| 16:00 | 4447 | Ruvu Shooting vs Mbeya City | 2.70 | 3.10 | 2.40 |
| 16:00 | 4519 | Simba vs Power Dynamos | 1.30 | 5.00 | 6.50 |
| 16:00 | 4752 | Vasteras SK vs Trelleborgs FF | 1.55 | 4.18 | 5.43 |
| 16:00 | 5852 | Fenerbahce vs Caykur Rizespor | 1.34 | 4.94 | 7.41 |
| 16:30 | 2398 | SV Darmstadt vs Werder Bremen | 2.79 | 3.66 | 2.39 |
| 16:30 | 3662 | Kryliya Sovetov vs Spartak Moscow | 2.81 | 3.48 | 2.24 |
| 16:30 | 4766 | TS Galaxy FC vs Richards Bay FC | 2.10 | 2.83 | 3.85 |
| 17:15 | 5048 | Alaves vs Osasuna | 2.69 | 3.05 | 2.85 |
| 17:30 | 2326 | FC Basel vs FC Stade LS Ouchy | 1.69 | 3.91 | 4.22 |
| 17:30 | 3816 | FC Arouca vs GD Chaves | 1.77 | 3.63 | 4.08 |
| 17:30 | 4899 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.22 | 3.46 | 2.89 |
| 18:00 | 1578 | Austria Vienna vs Rapid Vienna | 2.43 | 3.39 | 2.49 |
| 18:00 | 3623 | Molde vs Viking | 1.70 | 4.09 | 3.98 |
| 18:05 | 3756 | Lorient vs Montpellier | 2.94 | 3.50 | 2.36 |
| 18:30 | 1052 | Mjallby vs IFK Varnamo | 2.08 | 3.13 | 3.23 |
| 18:30 | 2328 | SC Freiburg vs Augsburg | 1.73 | 4.01 | 4.52 |
| 18:30 | 3026 | Hammarby vs IFK Goteborg | 1.73 | 3.52 | 4.03 |
| 19:00 | 2253 | Akhmat Grozny vs Dinamo Moscow | 2.52 | 3.39 | 2.51 |
| 19:00 | 2416 | Dynamo Kiev vs Oleksandria | 1.35 | 4.33 | 7.25 |
| 19:00 | 2671 | Konyaspor vs Besiktas | 3.10 | 3.46 | 2.11 |
| 19:00 | 3052 | Atalanta vs Juventus | 2.47 | 3.44 | 2.82 |
| 19:00 | 3522 | Hajduk Split vs Dinamo Zagreb | 2.72 | 3.17 | 2.34 |
| 19:00 | 3591 | Viborg FF vs Aarhus | 2.67 | 3.22 | 2.57 |
| 19:30 | 2965 | Brugge vs St Truiden | 1.37 | 4.66 | 7.14 |
| 20:00 | 1005 | CD Feirense vs Pacos Ferreira | 2.92 | 3.27 | 2.24 |
| 20:00 | 5949 | Vitoria Guimaraes vs GD Estoril | 1.78 | 3.53 | 4.17 |
| 20:15 | 2772 | Bodo Glimt vs Stromsgodset | 1.20 | 6.60 | 10.31 |
| 20:30 | 3782 | PAS Giannina vs Olympiakos | 7.28 | 4.06 | 1.45 |
| 21:45 | 3912 | Rennes vs Nantes | 1.51 | 4.53 | 5.97 |
| 21:45 | 5599 | Roma vs Frosinone | 1.48 | 4.34 | 7.02 |
| 22:00 | 2981 | Betis vs Valencia | 2.31 | 3.29 | 3.19 |
| 22:00 | 5609 | Atletico Madrid vs Cadiz CF | 1.37 | 4.96 | 8.27 |
| 22:30 | 5765 | Rio Ave vs Moreirense | 2.27 | 3.18 | 3.03 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo


Jumapili Oktoba 1, 2023

Nipashe




## Antony kuanza mazoezi Man Utd

UK. 22



Winga wa Yanga, Jesus Moloko (kushoto) akiwania mpira na beki wa Al Merrikh katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika jana kwenye uwanja wa Azam Complex Dar es Salaam, Yanga alishinda bao 1-0. **PICHA: SALEHJEMBE**

## Ni zamu ya Simba SC, Singida FG CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya jana kushuhudia mabingwa wa soka nchini, Yanga ikifuzu hatua ya makundi ya ligi ya Mabingwa Afrika, leo ni zamu ya wawakilishi wengine Simba na Singida Fountain Gate kusaka nafasi ya kutinga katika hatua hiyo.

Simba ikiwa kwenye uwanja wa Azam Complex leo itawakaribisha Power Dynamos kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya mabingwa Afrika wakati Singida Fountain Gate wakiwa ugenini Misri watasaka nafasi ya kutinga katika hatua hiyo kwenye Kombe la shirikisho Afrika.

Simba wakiwa nyumbani leo wanatakiwa kumfunga Power Dynamos katika mchezo huo utakaoanza saa 10:00 jioni au kutoka sare isiyozidi mabao 1-1 kuweza kutinga hatua ya makundi.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Ndola, Simba ililazimisha sare ya mabao 2-2 na Mabingwa hao wa Zambia na kuwaweka kwenye nafasi nzuri ya kufuzu hatua hiyo kwenye mchezo wa leo wa marudiano.

Katika mchezo wa leo Simba itawakosa nyota wake watatu kutokana na kuwa majeruhi akiwemo golikipa namba moja Aishi Manula, Aubin Kramo na Henock Inonga ambao wanaendelea kupatiwa matibabu.

Kocha Mkuu Roberto Oliveira 'Robertinho'

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yatinga makundi Afrika

### ●●● Ni ya Ligi ya mabingwa Afrika baada ya miaka 25 kupita, yaipiga Al Merrikh nje ndani..

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA imeandikwa, ndio.., ni baada ya jana Yanga kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya miaka 25 kupita ikiwa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Bao pekee la dakika ya 66 lililofungwa na Clement Mzize liliifanya timu hiyo kuondoka na ushindi wa bao 1-0 dhidi Al Merrikh ya Sudan na kuweka rekodi hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1998.

Yanga ambayo msimu uliopita ilifika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, imetinga hatua hiyo kwa jumla ya mabao 3-0 baada ya ushindi wa mabao 2-0 kwenye mchezo wao wa kwanza uliochezwa Kigali, Rwanda Septemba 16.

Mzize ameweka rekodi ya kufunga mabao kwenye mechi zote tatu za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Alifunga katika mechi ya marudiano dhidi ya ASAS ya Djibouti Agosti 26, Yanga ikishinda mabao 5-1, na kwenye mechi ya Septemba 16 dhidi ya Merrikh alifunga bao la pili dakika ya 78.

**Mpaka gazeti hili linaenda mtamboni jana, Yanga ilikuwa timu ya sita kutinga hatua ya makundi, ikiungana na Pyramids na Al Ahly za Misri, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jwaneng Galaxy ya Botswana na Petro de Luanda ya Angola, huku mechi nyingine zikichezwa leo.**

Kocha Mkuu wa Yanga Miguel Gamondi raia wa Argentina anakuwa kocha ya kwanza kupeleka klabu hiyo kwenye hatua ya makundi baada Mtanzania, Tito Mwaluvanda (marehemu), aliyefanya hivyo mwaka 1998 baada ya kuichapa Coffee ya Ethiopia mabao 6-1 Uwanja wa Taifa, Dar es salaam, mechi iliyochezwa Mei 8 mwaka huo.

Ilitinga hatua hiyo kwa jumla ya mabao 8-3, baada ya mechi ya kwanza ugenini iliyochezwa Aprili 26 mwaka huo nchini Ethiopia Yanga kulazimisha sare ya mabao 2-2.

Katika mchezo wa jana Yanga iliianza mechi kwa kasi na iliwachukua dakika nne kupata faulo nje kidogo ya eneo la hatari iliyotokana na Stephane Aziz Ki kufanyiwa madhambi.

Ni yeye mwenyewe aliyepiga faulo hiyo iliyowababatiza miguuni mabeki wa Al Merrikh na kurejea uwanjani.

Wageni walijibu mapigo dakika ya 12 kwa shambulio la kushtukiza kupitia kwa Bakhit Khamis ambaye alikuwa akielekea kufunga lakini beki wa kati wa Yanga Ibrahim Hamad 'Bacca' aliutokea mpira na na kuuokoa.

Kona iliyopigwa muda huo huo na Brayan Angulo nusura izae bao, kwani baada ya kuokolewa na Diarra ilimkuta naodha Muhamed Alrasheed aliyepiga shuti kali lakini lilienda pembeni kidogo mwa lango.

Dakika moja baadaye, Yanga ilirejea kwenye lango la wageni wao kwa shambulizi kali lililoanzia kwa Maxi Nzengeli aliyekokota mpira kwa umbali mrefu wingi ya kulia na kupiga krosi iliyoleta kizaazaa langoni mwa Al Merrikh, lakini mpira wa mwisho kupigwa na Kennedy Musonda uliokolewa kwa miguu na kipa Mohamed Mustapha.

Diarra alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika ya 20 kwa kuokoa mpira wa faulo iliyopigwa na Bakhit Khamis, huku Ahmed Al-Tash akikosa bao baada ya kupiga kichwa cha mbizi na mpira kutoka nje kidogo ya goli.

Mpaka timu hizo zinaenda mapumziko hazikuwa zimefungana.

Kipindi cha pili Yanga ilibadilika na kucheza mpira wa kasi ikisukuma mashambulizi mfululizo katika lango la wapinzani na hasa baada ya kuingia kwa Mzize aliyechukua nafasi ya Kennedy Musonda huku Salum Aboubakar akiingia kuchukua nafasi ya Khalid Aucho.

Yanga pia ilimtoa Aziz Ki na nafasi yake kuchukuliwa na Pacome, mabadiliko hayo yaliimarisha zaidi Yanga ambao walitawala mchezo kwa muda mrefu.

Yanga sasa itasubiri kujua atapangwa kwenye kundi gani na timu zipi katika droo itakayochezeshwa hivi karibuni ya Shirikisho la soka Afrika, CAF.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >